Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.

Budget Documents Budget Guidelines

2024-12

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025-2026

The United Republic of Tanzania

Ministry of Finance

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/846

Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26

DISEMBA 2024

YALIYOMO

VIFUPISHO ..... **i**
MUHTASARI II
1. MUHTASARI WA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24 ..... **1**
1.1 Utangulizi 1
1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi 1
1.3 Deni la Serikali 4
1.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24 4
1.5 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Robo ya Kwanza ya Mwaka 2024/25 5
2. VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 ..... **6**
2.1 Vipaumbele Mahsusi kwa Mwaka 2025/26 6
2.2 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla 7
2.3 Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 8
3. USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI **18**
3.1. Utangulizi 18
3.2. Vihatarishi vya Mpango na Bajeti 18
3.2.1. Vihatarishi vya Uchumi Jumla 18
3.2.2. Madeni Sanjari 19
3.2.3. Mabadiliko ya Tabianchi na Majanga ya Asili 19
3.2.4. Migogoro ya Kisiasa na Mahusiano ya Kidiplomasia 19
3.2.5. Udukuzi na Shambulio la Mifumo ya Kielektroniki 19
3.3. Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi 20
4. MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 ..... **22**
4.1 Maandalizi ya Mpango na Bajeti 22
4.2 Maelekezo ya Uandaaji wa Mpango na Bajeti 25
4.3 Maelekezo Mahsusi kwa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma 30
4.4 Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 31
4.5 Masuala Mengine Muhimu ya Kuzingatiwa Wakati wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti 35
4.6 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ... 39
4.7 Maelekezo kuhusu Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu 40

VIFUPISHO

AFDP	Agriculture and Fisheries Development Programme
ASDP	Agriculture Sector Development Programme
BBT	Building Better Tomorrow
CBR	Central Bank Rate
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CSR	Corporate Social Responsibility
DCF	Development Co-operation Framework
EAC	East African Community
EFD	Electornic Fiscal Device
EPZ	Export Processing Zone
GIS	Geographical Information System
GFS	Government Finance Statistics
GoT HOMIS	Government of Tanzania Health Operation Management Information System
HCMIS	Human Capital Management Information System
IMF	International Monetary Fund
MTEF	Medium Term Expenditure Framework
MCC	Millenium Challenge Corporation
MTAKUWWA	Mpangokazi wa Pili wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto
NeST	National e-Procurement System of Tanzania
NMNAP	National Multi-Sectoral Nutrition Action Plan
NMSF	National Multi-Sectoral Strategic Framework
OR - MUUUB	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora
OR - TAMISEMI	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PFMRP	Public Finance Management Reform Programme
PPP	Public Private Partnership
REGROW	Resilience Natural Resources for Tourism Growth
SMT	Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
SMZ	Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
SADC	Southern African Development Community
SEZ	Special Economic Zone
TDV	Tanzania Development Vision
TARURA	Tanzania Rural and Urban Roads Agency
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
VAT	Value Added Tax
VVU	Virusi Vya Ukimwi
WEO	World Economic Outlook

MUHTASARI

Mwongozo wa Mpango na Bajeti umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo wa Mwaka 2025/26 ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (TDV 2025) pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Maandalizi ya Mpango na Bajeti yamezingatia: Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi ya Mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na maelekezo mahsusi ya Serikali. Lengo la Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni kutoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wote kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2025/26 .

Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na maelekezo kuhusu ulazima wa kuzingatia vipaumbele vya mpango; maelekezo ya ujumla kuhusu uandaaji wa Mpango na Bajeti; Maelekezo mahususi kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma. Maeneo mengine ni, usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango ikijumuisha uainishaji, mikakati na hatua stahiki; ufuatiliaji na tathmini; uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi; na masuala ya Muungano. Mwongozo umegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni: Muhtasari wa mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi; vipaumbele vya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26; na maelekezo ya maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26. Mwongozo huu unapaswa kusomwa pamoja na viambatisho vyake vyote.

Utekelezaji wa maelekezo ya Mwongozo huu kwa ukamilifu utachangia: udhibiti wa matumizi ya fedha za umma na kuleta tija iliyokusudiwa; kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kutoa fursa sawa za ajira kwa wote; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili; kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; kuendelea kuongeza upatikanaji wa huduma za jamii kwa wote na uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani. Hivyo, Maafisa Masuuli wote wanasisitizwa kuzingatia maelekezo ya mwongozo huu kwa ukamilifu.

1. MUHTASARI WA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

1.1 Utangulizi

1. Sura hii inaelezea mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia, kikanda na Tanzania kwa mwaka 2023 na mwelekeo wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2024 hadi mwaka 2025, deni la Serikali pamoja na mapitio ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2023/24 na utekelezaji wa bajeti kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024/25.

1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi

1.2.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Kikanda

2. Uchumi wa dunia umeendelea kukua licha ya kukabiliana na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei, migogoro ya kisiasa hususan Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati, kuongezeka kwa bei za bidhaa za petroli, gharama kubwa za mikopo na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF *World Economic Outlook* – WEO, toleo la Julai 2024, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.2 mwaka 2024 na asilimia 3.3 katika mwaka unaofuatia.

3. Katika nchi zilizoendelea, taarifa ya WEO inaonesha uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 1.7 na asilimia 1.8 mwaka 2024 na 2025, mtawaliwa. Uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea ulikua kwa wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2022. Uchumi wa nchi hizo unatarajiwa kukua wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2024 na 2025. Uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikua kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2022 na unatarajiwa kukua wa asilimia 3.7 mwaka 2024 na asilimia 4.1 mwaka 2025. Uchumi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ulikua kwa wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2022. Uchumi wa nchi hizo unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.7 na asilimia 3.9 mwaka 2024 na 2025, mtawaliwa.Kwa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2024 na asilimia 6.1 mwaka 2025.

1.2.2 Ukuaji wa uchumi wa Tanzania

4. Shughuli za kiuchumi zimeendelea kuimarika licha ya kukabiliana na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika nchi zilizoendelea, migogoro ya kikanda, kuongezeka kwa bei za bidhaa za petroli, gharama kubwa za mikopo na mabadiliko ya tabianchi. Pato halisi la Taifa

lilifikia shilingi bilioni 148,399.76 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 141,247.19 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 5.1 ikilinganishwa asilimia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kilimo, ujenzi na uchimbaji madini. Viashiria vya kiuchumi kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2024 vinaonesha uchumi kuendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazoendelea za kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, Pato halisi la Taifa kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2024, lilikua kwa wastani wa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hivyo, Pato halisi la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2025 na asilimia 6.1 mwaka 2026. Ukuaji huu utategemea utekelezaji endelevu wa miradi mikubwa ya kimkakati inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji, jitihada za Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji, utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili – ASDP II, pamoja na uwekezaji wa Serikali katika sekta za kijamii.

1.2.2.1 Mfumuko wa Bei

5. Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.2 mwaka 2023/24, kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la nchi la asilimia 5.0 na sawia na malengo ya mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Aidha, kiwango hicho kilikuwa chini ya asilimia 4.7 kwa mwaka 2022/23. Kupungua huko kulitokana na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti, kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, na utoshelevu wa chakula nchini. Mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la nchi la asilimia 5, ukichangiwa na matarajio ya upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, kuimarika kwa upatikanaji wa umeme hususan kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, utulivu wa bei za bidhaa katika soko la dunia pamoja na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti.

1.2.2.2 Utekelezaji wa Sera ya Fedha

6. Matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha yalikuwa ya kuridhisha, licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali, hususan zilizotokana na mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia na uhaba wa fedha za kigeni. Januari 2024, Benki Kuu ilianza kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate - CBR), lengo likiwa ni kuongeza ufanisi wa sera ya fedha ili kuendana na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi. Utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia mfumo huu utachangia katika kuongeza ukuaji wa shughuli za kiuchumi kutokana na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa imara, licha ya kasi ya ukuaji kupungua. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 18.1 katika mwaka 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 22.2 mwaka 2022/23. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi lilichangiwa zaidi na mikopo iliyoelekezwa kwenye kilimo, uchimbaji madini, uchukuzi na mawasiliano, shughuli binafsi na uzalishaji viwandani.

1.2.2.3 Viwango vya Riba

7. Riba za dhamana za Serikali ziliongezeka hadi wastani wa asilimia 9.14 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 5.73 mwaka 2022/23. Hali hii ilitokana na kupungua kwa ukwasi (tight financial conditions) katika masoko ya fedha, kama ilivyokuwa katika nchi nyingine kufuatia benki kuu duniani kutekeleza sera ya fedha kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei. Riba za mikopo zilipungua hadi wastani wa asilimia 15.47 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 16.04 mwaka 2022/23. Riba za amana ziliongezeka hadi asilimia 7.32 kutoka asilimia 7.16 mwaka 2022/23. Riba za mikopo kwa sekta binafsi zinatarajiwa kupungua kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha sekta ya fedha pamoja na matarajio ya kuwa na mfumuko wa bei mdogo nchini.

1.2.2.4 Viwango vya Ubadilishaji Fedha

8. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kwa wastani wa asilimia 8.5 kwa mwaka 2023/24, ikilinganishwa na takriban asilimia moja kwa mwaka 2022/23. Kupungua huko kulitokana na uhaba wa fedha za kigeni nchini uliotokana na uamuzi wa benki kuu za nchi zilizoendelea kupandisha riba ili kukabiliana na mfumuko wa bei pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan bidhaa za petroli kulikosababisha ongezeko kubwa la mahitaji ya fedha za kigeni. Thamani ya shilingi inatarajiwa kuimarika kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni pamoja na katazo la matumizi ya fedha za kigeni katika kufanya malipo nchini.

1.2.2.5 Sekta ya Fedha

9. Katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Huduma Jumuishi za Kifedha (2023 – 2028), Serikali imeimarisha mifumo ya malipo ya kielektroniki na matumizi ya simu za mkononi katika huduma za kifedha. Aidha, ili kuimarisha huduma jumuishi za fedha, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya fedha kwa kutoa elimu na kufanya tafiti kuhusu hali ya huduma za kifedha nchini.

10. Benki za biashara zimeendelea kuimarika na kutengeneza faida zikiwa na viwango vya kutosha vya mitaji na ukwasi, ambapo kwa mwaka 2023/24 faida ya benki za biashara ilikuwa shilingi bilioni 1,060.87. Aidha, mikopo chechefu ilipungua hadi asilimia 4.1 kutoka asilimia 5.3 mwaka 2022/23. Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa katika kipindi kilichoishia Juni 2024 uliongezeka kwa asilimia 12.1 na kufikia shilingi bilioni 16,834.28 ikilinganishwa na shilingi bilioni 15,010.36 katika kipindi kilichoishia Juni 2023. Aidha, mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 153.4 na kufikia shilingi bilioni 272.69 ikilinganishwa na shilingi bilioni 107.61 katika kipindi kilichoishia Juni 2023. Vilevile, mali za soko la bima (assets) ziliongezeka kwa asilimia 25.9 kufikia shilingi bilioni 2,144 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,679 mwaka 2022 ambapo wanufaika wa huduma za bima waliongezeka kwa asilimia 32.0. Ongezeko hilo linatokana na Serikali kuendelea kutoa elimu ya masuala ya bima kwa jamii.

1.2.2.6 Sekta ya Nje

11. Sekta ya nje iliendelea kuimarika ikilinganishwa na mwaka 2022/23, kutokana na kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi yatokanayo na utalii, dhahabu na bidhaa asilia pamoja na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Kwa mwaka 2023/24, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,345.5, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa takribani miezi 4.4. Kiasi hiki ni zaidi ya shabaha ya nchi ya miezi minne (4) ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Sekta ya nje inatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na kupungua kwa athari za mitikisiko ya kiuchumi duniani, ambapo nakisi ya urari wa malipo ya kawaida (current account deficit) inakadiriwa kupungua hadi kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka ulioishia Septemba 2024 kutoka asilimia 4.4 ya Pato la Taifa katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Mwenendo huu ulitokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan utalii, dhahabu, tumbaku, korosho, na bidhaa za mbogamboga na maua.

1.3 Deni la Serikali

12. Hadi Juni 2024, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 96,884.18 ikilinganishwa na shilingi bilioni 81,980.26 Juni 2023. Kati ya deni hilo, deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 64,932.94 na deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 31,951.24. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Juni 2024 imeonesha kuwa deni ni himilivu na viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Aidha, mwaka 2023/24, kampuni za Fitch Ratings na Moody’s Investors Service zilifanya mapitio ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa na kuchapisha matokeo ya daraja B1 na B+ mtawalia. Matokeo mazuri ya tathmini hizo yalitokana na ukuaji mzuri wa uchumi unaoweza kuhimili mitikisiko ya kiuchumi, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha mazingira ya biashara, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma.

1.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24

13. Katika mwaka 2023/24, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi bilioni 44,338.07. Katika kipindi hicho, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 42,920.62 sawa na asilimia 96.7 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 29,829.89 mapato ya ndani sawa na asilimia 95.1 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 31,381.01; shilingi bilioni 5,581.61 ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 102.1 ya lengo la shilingi bilioni 5,466.21; na shilingi bilioni 7,509.11 ni mikopo ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi sawa na asilimia 99.6 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 7,540.84.

14. Katika kipindi hicho, Serikali imetumia shilingi bilioni 42,945.21 kugharamia utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya Serikali ikiwemo miradi ya kimkakati na kielelezo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 28,308.79 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 14,636.42 ni matumizi ya maendeleo. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 24.59 kiligharamiwa kwa mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ambao upo ndani

wigo unaokubalika kisheria. Maelezo ya kina yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1C**.

1.5 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Robo ya Kwanza ya Mwaka 2024/25

15. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, Serikali imekusanya shilingi bilioni 11,553.33 kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 7,930.02 ni mapato ya ndani, sawa na asilimia 99.4 ya lengo la shilingi bilioni 7,976.35. Misaada na mikopo nafuu ilifikia shilingi bilioni 1,373.09, sawa na asilimia 118.5 ya lengo la shilingi bilioni 1,159.18. Aidha, mikopo ya kibiashara kutoka masoko ya ndani ilifikia shilingi bilioni 1,656.56, sawa na asilimia 97.8 ya lengo la shilingi bilioni 1,694.35. Mikopo ya kibiashara kutoka nje ilifikia shilingi bilioni 593.65, sawa na asilimia 79.5 ya lengo la shilingi bilioni 746.78.

16. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25, ridhaa ya shilingi bilioni 11,667.53 ilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 7,549.62 na matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 4,117.91. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 114.20 kiligharamiwa kwa mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ambao upo ndani wigo unaokubalika kisheria.

2. VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

17. Mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambavyo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza ujuzi.

2.1 Vipaumbele Mahsusi kwa Mwaka 2025/26

Kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo, maeneo mahsusi yatakayopewa kipaumbele cha bajeti kwa mwaka 2025/26 ni:

(i) **Uendelezaji wa Miundombinu:** Uendelezaji wa miundombinu ya usafirishaji, maji, nishati na TEHAMA ili kuwezesha mageuzi ya viwanda na kuchochea biashara na kuimarisha ushiriki wa nchi katika utangamano wa kikanda. Baadhi ya miradi itakayoendelea kupewa kipaumbele ni: ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme na uimarishaji wa gridi ya Taifa, usambazaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pamoja na ujenzi wa madaraja na barabara.

(ii) **Mapinduzi ya Sekta ya Kilimo:** Eneo hili litajielekeza katika uboreshaji wa kilimo ikiwemo matumizi ya teknolojia na mbinu za kisasa, tafiti na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Lengo ni kuongeza tija, kuimarisha usalama na utoshelevu wa chakula nchini, kuimarisha upatikanaji wa masoko na kuongeza kipato cha wakulima, wafugaji na wavuvi. Baadhi ya programu zitakazopewa kipaumbele ni: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II, Programu ya Mifumo Himilivu ya Chakula, Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora – BBT na Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi – AFDP.

(iii) **Uzalishaji Viwandani:** Msukumo utawekwa katika kuongeza thamani ya uzalishaji viwandani kwa kuchochea upatikanaji na matumizi ya teknolojia za kisasa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya mitaa ya viwanda (industrial clusters), upatikanaji wa fedha na mitaji, kuimarisha masoko ya bidhaa za viwandani na kuendeleza miundombinu ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ na EPZ).

(iv) **Uendelezaji wa Sekta ya Madini:** Eneo hili litajielekeza katika uboreshaji wa sekta ya madini kwa: Kufanya tafiti na ugani wa jiosayansi ikiwemo utafiti wa kina wa jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege (high resolution airborne geophysical survey) kwa ajili ya kukusanya taarifa za hali ya madini nchini; uendelezaji wa miradi ya madini muhimu na madini mkakati; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi wakiwemo wachimbaji wadogo kwenye uchumi wa madini; na kuimarisha mifumo ya usimamizi, ukaguzi na biashara ya madini ili kuongeza mapato

kwa kudhibiti utoroshaji wa madini na ukwepaji kodi.

(v) **Uendelezaji wa Sekta ya Utalii:** Kukuza utalii endelevu ili kupanua shughuli za kiuchumi na kuongeza mapato ya fedha za kigeni kupitia uendelezaji wa miundombinu ya utalii, kuibua mazao mapya ya utalii, kutangaza vivutio vya kipekee vya Tanzania na uhifadhi wa mazingira ikiwemo utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuendeleza utalii.

(vi) **Kukuza Sekta ya Fedha:** Kuimarisha upatikanaji wa huduma za fedha kwa kuwezesha uendelezaji wa bidhaa na huduma mbalimbali za fedha ikiwemo upatikanaji wa mikopo kwa gharama nafuu, ukuzaji wa masoko ya mitaji na uendelezaji wa huduma za bima.

(vii) **Kuongeza wigo wa Kinga ya Jamii:** Kutoa kinga ya jamii kwa makundi yaliyo katika hali hatarishi kutokana na umaskini, uzee, ulemavu na majanga na kuongeza idadi ya wanufaika hususan kutoka katika sekta isiyo rasmi ili kuhakikisha ustawi wa jamii yote na kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa mpango wa bima ya afya kwa wote.

(viii) **Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi:** Kutekeleza sera za hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa lengo la kuimarisha hifadhi ya bionuwai, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ili kuwezesha ukuaji endelevu wa uchumi na kupunguza uharibifu wa Mazingira. Hii inajumuisha utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032) pamoja na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034).

(ix) **Utawala na Maboresho ya Kitaasisi:** Kuboresha usimamizi na mifumo ya kitaasisi ili kuimarisha utawala bora kwa kupambana na vitendo vya rushwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji pamoja na kujenga taasisi imara zinazosimamia utawala wa sheria.

(x) **Kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa makundi maalum:** Msukumo utawekwa katika kutoa fursa sawa kwa makundi maalum ili kunufaika na fursa za kiuchumi na kijamii.

2.2 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla

2.2.1 Shabaha za Uchumi Jumla

18. Shabaha na malengo ya uchumi jumla yatakayozingatiwa kwa mwaka 2025/26 ni:

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.8 mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia 6.1 mwaka 2026;

(ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 16.1 na mapato ya kodi asilimia 13.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025/26; na
(iv) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

2.2.2 Misingi ya Uchumi Jumla

19. Misingi iliyotumika katika kuandaa malengo ya uchumi jumla ni pamoja na:
(i) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;
(ii) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na biashara;
(iii) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko)
(iv) Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na
(v) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi na katika nchi jirani.

2.3 Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26

20. Mwaka 2025/26, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia shilingi bilioni 55,061.61 ili kugharamia utekelezaji wa mpango na bajeti.

2.3.1 Mapato ya Ndani

21. Mwaka 2025/26, mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 38,962.49. Kati ya mapato hayo, mapato ya kodi ni shilingi bilioni 31,426.12, mapato yasiyo ya kodi ni shilingi bilioni 5,976.57 na mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni shilingi bilioni 1,559.79. Katika kipindi cha muda wa kati, mapato ya ndani yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 11.2 na kufikia shilingi bilioni 47,551.76 mwaka 2027/28. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti unakadiriwa kuwa asilimia 70.8 mwaka 2025/26 na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 76.2 mwaka 2027/28. Mchanganuo wa mapato ya ndani kwa muda wa kati ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 2.1.**

Kielelezo Na 2.1: Mchanganuo wa Mapato ya Ndani katika Muda wa Kati (Shilingi Bilioni)



2.3.1.1 Mikakati na Hatua za Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Mikakati

(i) Kufanya tafiti, tathimini, na mapitio ya vyanzo vya mapato vilivyopo na kuboresha kanzidata ya walipakodi, ada na tozo za Serikali ili kubaini maeneo yenye upotevu na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato;

(ii) Kuanzisha vituo vya huduma za kodi kwenye maeneo yanayokua katika shughuli za kiuchumi ikiwemo biashara ndogondogo;

(iii) Kuunganisha mifumo ya kodi na mifumo ya taasisi nyingine za umma ili kupata taarifa zitakazowaibua walipakodi ambao hawajasajiliwa ili kuwaingiza kwenye mfumo rasmi wa kodi;

(iv) Kutanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuibua vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuweka mbinu za kurahisisha utambuzi, usajili, ukadiriaji na ulipaji wa kodi, ada na tozo za Serikali;

(v) Kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa walipakodi kwa kutumia Mfumo wa Vitalu vya Walipakodi unaotumia teknolojia ya Mfumo wa Taarifa wa Kijiografia – Geographical Information System (GIS);

(vi) Kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu matumizi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki - EFD kupitia uendeshaji wa programu mbalimbali za hamasa ikiwemo Tunu ya Uzalendo;

(vii) Kuhakikisha taasisi zenye mlengo wa utoaji huduma kwa pamoja zinaboresha mifumo ya ukusanyaji kwa kutoa namba ya malipo jumuishi ili kurahisisha ulipaji wa kodi, ada na tozo kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji wa mapato ya Serikali;

(viii) Kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya teknolojia na kuboresha

ushirikiano wa pamoja kwa taasisi za Serikali zinazokusanya mapato kwa lengo la kubadilishana taarifa na mbinu za ukusanyaji ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi;

(ix) Kukabiliana na vitendo vya ukwepaji kodi kwa kuimarisha upatikanaji wa taarifa na kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wa umma, hususan kwenye maeneo ya ukaguzi na uchunguzi;

(x) Kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa ada na tozo mbalimbali kwenye shughuli za kiuchumi zinazokua ikiwemo sekta ya ardhi, uvuvi, misitu, mifugo na ujenzi na hivyo kuwa na fursa kubwa ya mapato;

(xi) Kuboresha utozaji wa vyanzo vya mapato vinavyotozwa na mamlaka za udhibiti kwa kushughulikia dosari na malalamiko yanayotolewa na wananchi;

(xii) Kuhamasisha na kuhimiza matumizi ya malipo ya kidigitali ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu; na

(xiii) Kufanya mapitio ya vivutio vya kodi/misamaha ya kodi iliyotolewa ili kubaini faida na umuhimu wa kuendelea nayo au vinginevyo.

Hatua

(i) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini katika sekta za huduma na uzalishaji ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi;

(ii) Kuongeza wigo kwa kutambua vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuongeza idadi ya walipakodi;

(iii) Kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato ya ndani;

(iv) Kuandaa mpango na mkakati wa kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi katika Wizara, Idara, Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(v) Kuendelea kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi ili wawe na motisha ya ulipaji wa kodi, tozo na ada kwa Serikali kwa hiari;

(vi) Kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi; na

(vii) Kuendelea kuboresha utendaji wa mashirika ya umma ili kuongeza mchango wake katika mapato.

2.3.2 Misaada

22. Katika mwaka 2025/26, misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1,024.88, sawa na ongezeko la asilimia 29.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 794.39 zilizoahidiwa mwaka 2024/25. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa ahadi za fedha za misaada kwenye programu ya *Millenium Challenge Corporation* (MCC), Mfuko wa Sekta ya Afya na Mfuko wa Usimamizi wa Fedha za Umma - PFMRP. Katika kipindi cha muda wa kati, fedha za misaada zinatarajiwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 6.9.

2.3.2.1 Mikakati ya Upatikanaji wa Misaada

23. Serikali itaendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kupitia Majadiliano ya

Kimkakati (Strategic Dialogue) yanayolenga kuainisha vipaumbele vya Serikali ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za misaada kama ilivyopangwa. Vilevile, Serikali itaendelea kutekeleza mambo yafuatayo:

(i) Kuhamasisha Washirika wa Maendeleo kutoa fedha za misaada moja kwa moja Serikalini bila kupitia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza tija ya fedha hizo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali; na

(ii) Kuendelea kutenga sehemu ya bajeti ya Serikali (counterpart fund) kwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo.

2.3.3 Matumizi

24. Matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 55,061.61 kwa mwaka 2025/26, sawa na ongezeko la asilimia 11.6 kutoka shilingi bilioni 49,345.69 mwaka 2024/25. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 38,602.18 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 16,459.43. Matumizi ya kawaida yanajumuisha gharama kwa ajili ya: deni la Serikali shilingi bilioni 14,208.98; mishahara shilingi bilioni 13,454.24; huduma za Mfuko Mkuu na uendeshaji wa shughuli za Serikali shilingi bilioni 9,496.92; na ruzuku ya maendeleo shilingi bilioni 1,442.04 kwa ajili ya Programu ya Elimumsingi na Sekondari Bila Ada na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha shilingi bilioni 11,508.53 fedha za ndani na shilingi bilioni 4,950.90 fedha za nje. Vilevile, katika kipindi cha muda wa kati, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 8.2. Mchanganuo wa makadirio ya matumizi ya Serikali umeanishwa katika **Jedwali Na. 2.1 hadi 2.5**.

2.3.3.1 Mikakati ya Usimamizi wa Matumizi

25. Mikakati ya usimamizi wa matumizi katika kipindi cha muda wa kati itajumuisha yafuatayo:

(i) Kuendelea kusimamia na kuimarisha matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kudhibiti matumizi ikijumuisha mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu, malipo serikalini, ununuzi na usimamizi wa mali za Serikali;

(ii) Kuelekeza fedha katika kutekeleza miradi ya kimkakati yenye tija kubwa katika uchumi na ustawi wa jamii na kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya;

(iii) Kuimarisha uwajibikaji na udhibiti katika matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma ili kuziba mianya ya ubadhilifu kwa lengo la kupata thamani ya fedha katika matumizi ya Serikali;

(iv) Kuimarisha mfumo wa usimamizi na utendaji kazi katika taasisi na mashirika ya umma;

(v) Kuunganisha mifumo ili kuiwezesha kubadilishana taarifa za kibajeti;

(vi) Kuendelea kukuza na kuimarisha ushirikiano wa kisekta ili kuepuka rasilimali kutumika kutekeleza jukumu linalofanana katika wizara/taasisi zaidi ya moja; na

(vii) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha inatekelezwa kwa ufanisi na kuokoa gharama za ziada zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji.

2.3.4 Kugharamia Nakisi ya Bajeti

26. Serikali itaendelea kugharamia nakisi ya bajeti kwa kutumia mikopo kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa kuzingatia Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali wa mwaka 2024. Katika mwaka 2025/26, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 15,074.24. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya ndani yenye masharti ya kibiashara ni shilingi bilioni 6,278.19, mikopo ya nje yenye masharti nafuu shilingi bilioni 5,667.04 na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 3,129.01. Fedha zitakazokopwa zitaelekezwa kwenye kugharamia miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi pamoja na hatifungani za Serikali zilizoiva.

Jedwali Na 2.1: Makadirio ya Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati 2024/25 - 2027/28 (Analytical Budget Frame)

Shilingi Bilioni

	2024/25 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI	2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI	2027/28 MAKADIRIO YA BAJETI
Jumla ya Mapato ya Ndani	**34,610.65**	**38,962.49**	**42,775.56**	**47,551.76**
Mapato ya Kodi	28,046.65	31,426.12	34,539.94	38,422.27
Mapato Yasiyo ya Kodi	5,207.66	5,976.57	6,503.69	7,241.69
Mapato ya Halmashauri	1,356.34	1,559.79	1,731.93	1,887.80
Jumla ya Matumizi*	**41,806.20**	**47,346.35**	**51,181.46**	**53,408.23**
Matumizi ya Kawaida	27,035.89	30,886.92	33,084.15	35,525.53
Malipo ya Riba Nje	2,435.31	2,796.43	2,887.75	2,947.26
Malipo ya Riba Ndani	3,146.67	3,697.29	3,965.08	3,965.08
Mishahara	11,767.99	13,454.24	14,304.24	15,154.24
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	2,000.00	2,428.49	2,608.99	2,807.54
Matumizi mengineyo	6,414.24	7,068.43	7,699.86	8,862.23
Ruzuku ya Maendeleo	1,271.69	1,442.04	1,618.23	1,789.18
-Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	787.42	931.07	1,051.56	1,160.75
-Elimumsingi na Sekondari Bila Ada	484.27	510.97	566.66	628.43
Matumizi ya Maendeleo	14,770.30	16,459.43	18,097.31	17,882.70
Fedha za Ndani	11,129.47	11,508.53	11,997.03	12,924.11
Fedha za Nje	3,640.84	4,950.90	6,100.28	4,958.59
Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada	**(7,195.55)**	**(8,383.86)**	**(8,405.90)**	**(5,856.47)**
Misaada	**794.39**	**1,024.88**	**1,087.30**	**930.58**
Misaada ya Kibajeti	109.02	113.80	105.83	100.52
Misaada ya Maendeleo	572.96	801.98	882.17	753.98
Mifuko ya Kisekta	112.41	109.11	99.29	76.08
Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada	**(6,401.16)**	**(7,358.97)**	**(7,318.61)**	**(4,925.89)**
Jumla ya Nakisi	**(6,401.16)**	**(7,358.97)**	**(7,318.61)**	**(4,925.89)**
Kuziba Nakisi	**6,401.16**	**7,358.97**	**7,318.61**	**4,925.89**
Kuziba Nakisi Kutoka Nje	**3,805.74**	**4,406.34**	**4,354.18**	**1,961.47**
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1,380.75	1,627.22	699.71	-
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	2,888.99	3,959.19	5,038.19	4,087.64
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	66.48	80.62	80.62	40.89
Mikopo ya Kibiashara	2,986.64	3,129.01	3,011.95	2,524.20
Malipo ya Mtaji Deni la Nje	(3,517.12)	(4,389.71)	(4,476.29)	(4,691.27)
Kuziba Nakisi Kutoka Ndani	**2,595.42**	**2,952.63**	**2,964.42**	**2,964.42**
Mkopo kwa ajili kugharamia miradi ya maendeleo (NDF)	**2,595.42**	**2,952.63**	**2,964.42**	**2,964.42**
Mkopo kwa ajili ya kulipa mtaji	4,022.37	3,325.56	4,192.89	4,318.68
Malipo ya Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	(4,022.37)	(3,325.56)	(4,192.89)	(4,318.68)
Pato Ghafi la Taifa	**218,779.14**	**242,071.49**	**267,419.82**	**297,420.82**

Chanzo: Wizara ya Fedha

*Tanbihi: Kiasi cha jumla ya matumizi hakijumuishi malipo ya mtaji

Jedwali Na 2.2: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato la Taifa kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2024/25 -2027/28 (Analytical Budget Frame)

	2024/25 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI	2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI	2027/28 MAKADIRIO YA BAJETI
Jumla ya Mapato ya Ndani	**15.8%**	**16.1%**	**16.0%**	**16.0%**
Mapato ya Kodi	12.8%	13.0%	12.9%	12.9%
Mapato Yasiyo ya Kodi	2.4%	2.5%	2.4%	2.4%
Mapato ya Halmashauri	0.6%	0.6%	0.6%	0.6%
Jumla ya Matumizi*	**19.1%**	**19.6%**	**19.1%**	**18.0%**
Matumizi ya Kawaida	12.4%	12.8%	12.4%	11.9%
Malipo ya Riba Nje	1.1%	1.2%	1.1%	1.0%
Malipo ya Riba Ndani	1.4%	1.5%	1.5%	1.3%
Mishahara	5.4%	5.6%	5.3%	5.1%
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	0.9%	1.0%	1.0%	0.9%
Matumizi mengineyo	2.9%	2.9%	2.9%	3.0%
Ruzuku ya Maendeleo				
-Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	0.4%	0.4%	0.4%	0.4%
-Elimumsingi na Sekondari Bila Ada	0.2%	0.2%	0.2%	0.2%
Matumizi ya Maendeleo	6.8%	6.8%	6.8%	6.0%
Fedha za Ndani	5.1%	4.8%	4.5%	4.3%
Fedha za Nje	1.7%	2.0%	2.3%	1.7%
Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada	**-3.3%**	**-3.5%**	**-3.1%**	**-2.0%**
Misaada	**0.4%**	**0.4%**	**0.4%**	**0.3%**
Misaada ya Kibajeti	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Misaada ya Maendeleo	0.3%	0.3%	0.3%	0.3%
Mifuko ya Kisekta	0.1%	0.0%	0.0%	0.0%
Nakisi ya Bajeti Ikijumuisha Misaada	**-2.9%**	**-3.0%**	**-2.7%**	**-1.7%**
Jumla ya Nakisi	**-2.9%**	**-3.0%**	**-2.7%**	**-1.7%**
Kuziba Nakisi	**2.9%**	**3.0%**	**2.7%**	**1.7%**
Kuziba Nakisi Kutoka Nje	**1.7%**	**1.8%**	**1.6%**	**0.7%**
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.6%	0.7%	0.3%	0.0%
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1.3%	1.6%	1.9%	1.4%
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Mikopo ya Kibiashara	1.4%	1.3%	1.1%	0.8%
Malipo ya Mtaji Deni la Nje	-1.6%	-1.8%	-1.7%	-1.6%
Kuziba Nakisi Kutoka Ndani	**1.2%**	**1.2%**	**1.1%**	**1.0%**
Mkopo kwa ajili kugharamia miradi ya maendeleo (NDF)	**1.2%**	**1.2%**	**1.1%**	**1.0%**
Mkopo kwa ajili ya kulipa mtaji	1.8%	1.4%	1.6%	1.5%
Malipo ya Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	-1.8%	-1.4%	-1.6%	-1.5%

Chanzo: Wizara ya Fedha

Jedwali Na 2.3: Makadirio ya Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati 2024/25 - 2027/28 (Accounting Budget Frame)

Shilingi Bilioni

	2024/25 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI	2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI	2027/28 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	**49,345.69**	**55,061.61**	**59,850.64**	**62,418.18**
Mapato ya Ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri	34,610.65	38,962.49	42,775.56	47,551.76
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1,489.77	1,741.02	805.54	100.52
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	3,461.95	4,761.17	5,920.37	4,841.62
Misaada na Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	178.89	189.74	179.92	116.97
Mikopo ya Ndani - Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	4,022.37	3,325.56	4,192.89	4,318.68
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara (NDF)	2,595.42	2,952.63	2,964.42	2,964.42
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	2,986.64	3,129.01	3,011.95	2,524.20
II. JUMLA YA MATUMIZI	**49,345.69**	**55,061.61**	**59,850.64**	**62,418.18**
Matumizi ya Kawaida	34,575.38	38,602.18	41,753.33	44,535.47
Mfuko Mkuu wa Serikali	15,736.28	17,340.28	18,921.81	19,608.64
o/w Malipo ya riba	5,581.97	6,493.72	6,852.83	6,912.34
o/w Malipo ya mtaji	7,539.49	7,715.26	8,669.18	9,009.95
Mishahara	11,767.99	13,454.24	14,304.24	15,154.24
Matumizi Mengineyo	5,799.42	6,365.62	6,909.05	7,983.41
Ruzuku ya Maendeleo	1,271.69	1,442.04	1,618.23	1,789.18
Matumizi ya Maendeleo	14,770.30	16,459.43	18,097.31	17,882.70
Fedha za Ndani	11,129.47	11,508.53	11,997.03	12,924.11
Fedha za Nje	3,640.84	4,950.90	6,100.28	4,958.59
Pato Ghafi la Taifa	**218,779.14**	**242,071.49**	**267,419.82**	**297,420.82**

Chanzo: Wizara ya Fedha

Tanbihi: Kiasi cha jumla ya matumizi kinajumuisha malipo ya mtaji

Jedwali Na 2.4: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato la Taifa kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2024/25 -2027/28 (Accounting Budget Frame)

	2024/25 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI	2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI	2027/28 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	**22.6%**	**22.7%**	**22.4%**	**21.0%**
Mapato ya Ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri	15.8%	16.1%	16.0%	16.0%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.7%	0.7%	0.3%	0.0%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	1.6%	2.0%	2.2%	1.6%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	0.1%	0.1%	0.1%	0.0%
Mikopo ya Ndani - Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	1.8%	1.4%	1.6%	1.5%
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara (NDF)	1.2%	1.2%	1.1%	1.0%
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	1.4%	1.3%	1.1%	0.8%
II. JUMLA YA MATUMIZI	**22.6%**	**22.7%**	**22.4%**	**21.0%**
Matumizi ya Kawaida	15.8%	15.9%	15.6%	15.0%
Mfuko Mkuu wa Serikali	7.2%	7.2%	7.1%	6.6%
o/w Malipo ya riba	2.6%	2.7%	2.6%	2.3%
o/w Malipo ya mtaji	3.4%	3.2%	3.2%	3.0%
Mishahara	5.4%	5.6%	5.3%	5.1%
Matumizi Mengineyo	2.7%	2.6%	2.6%	2.7%
Ruzuku ya Maendeleo	0.6%	0.6%	0.6%	0.6%
Matumizi ya Maendeleo	**6.8%**	**6.8%**	**6.8%**	**6.0%**
Fedha za Ndani	5.1%	4.8%	4.5%	4.3%
Fedha za Nje	1.7%	2.0%	2.3%	1.7%

Chanzo: Wizara ya Fedha

Jedwali Na 2.5: Mgawanyo wa Bajeti Kisekta kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2024/25 -2027/28

(Shilingi Bilioni)

SEKTA	2024/25 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2025/26 MAKADIRIO YA BAJETI	2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI	2027/28 MAKADIRIO YA BAJETI
1 - Elimu	**6,168.39**	**6,985.82**	**7,551.68**	**7,880.24**
1.1 - Elimu Msingi	4,395.26	4,977.72	5,380.93	5,615.04
1.2 - Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi	196.54	222.58	240.61	251.08
1.3 - Elimu ya Juu	1,347.03	1,525.54	1,649.11	1,720.85
1.4 - Sayansi, Teknolojia na Ubunifu	72.37	81.96	88.60	92.46
1.5 - Huduma za Utawala	157.19	178.02	192.44	200.81
2 - Afya	**2,540.89**	**2,877.60**	**3,110.69**	**3,246.03**
2.1 - Huduma za Tiba	1,062.38	1,203.16	1,300.62	1,357.21
2.2 - Huduma za Kinga	310.73	351.91	380.42	396.97
2.4 - Zahanati	61.02	69.10	74.70	77.95
2.5 - Vituo vya Afya	109.28	123.76	133.78	139.61
2.6 - Hospitali za Wilaya	901.82	1,021.33	1,104.06	1,152.09
2.7 - Huduma za Utawala	95.66	108.34	117.11	122.21
3 - Huduma za Utawala na Deni la Serikali	**13,237.71**	**14,917.61**	**15,959.07**	**16,653.41**
3.1 - Utawala na Bunge	5,068.05	5,493.29	5,938.25	6,196.61
3.2 - Usimamizi wa mapato na Matumizi	2,346.94	2,657.95	2,873.25	2,998.26
3.3 - Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa	240.75	272.66	294.74	307.56
3.4 - Deni la Serikali (Malipo ya Riba)	5,581.97	6,493.72	6,852.83	7,150.98
4 - Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama	**5,493.17**	**6,221.13**	**6,725.05**	**7,017.64**
4.1 - Ulinzi	3,323.46	3,763.89	4,068.77	4,245.79
4.2 - Usalama wa Umma	1,703.82	1,929.61	2,085.91	2,176.66
4.3 - Mahakama	465.89	527.63	570.37	595.19
5 - Maendeleo ya Uchumi	**10,291.02**	**11,729.14**	**12,846.09**	**13,405.00**
5.1 - Kilimo	1,938.94	2,195.89	2,373.76	2,477.04
5.2 - Madini	231.91	262.64	283.92	296.27
5.3 - Nishati	1,883.74	2,207.73	2,449.85	2,556.43
5.4 - Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	5,483.92	6,210.65	6,817.31	7,113.91
5.5 - Maliasili, Utalii na Mazingira	335.35	379.79	410.56	428.42
5.6 - Viwanda	111.15	125.88	136.07	141.99
5.7 - Biashara	272.01	308.06	333.01	347.50
5.8 - Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi	33.99	38.50	41.62	43.44
6 - Hifadhi ya Jamii	**2,653.44**	**3,005.07**	**3,248.49**	**3,389.82**
6.1 - Wazee, Watoto na Watu wenye Ulemavu	50.11	56.75	61.35	64.02
6.2 - Mifuko ya Hifadhi ya Jamii	2,157.07	2,442.93	2,640.81	2,755.70
6.3 - Mfuko wa Bima wa Afya	446.25	505.39	546.33	570.10
7 - Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii	**1,421.58**	**1,609.97**	**1,740.38**	**1,816.10**
7.1 - Maji	641.88	726.94	785.83	820.02
7.2 - Ardhi, Nyumba na Makazi ya Watu	174.09	197.16	213.13	222.41
7.3 - Maendeleo ya Jamii	320.32	362.76	392.15	409.21
7.4 - Habari, Michezo na Utamaduni	285.29	323.10	349.27	364.46
Jumla ya Sekta	**41,806.19**	**47,346.34**	**51,181.46**	**53,408.24**
Deni la Serilaki (Malipo ya Mtaji)	7,539.49	7,715.26	8,669.18	9,009.95
Jumla Kuu	**49,345.69**	**55,061.61**	**59,850.64**	**62,418.18**

Chanzo: Wizara ya Fedha

3. USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

3.1. Utangulizi

27. Katika uandaaji wa mpango na bajeti, Serikali huainisha vipaumbele katika utekelezaji wa mikakati mbalimbali ili kufikia malengo ya kitaifa. Hata hivyo, baadhi ya vihatarishi vinaweza kujitokeza na kuathiri utekelezaji wa mikakati husika katika hatua mbalimbali za usimamizi wa mpango na bajeti. Kwa muktadha huo, ni muhimu kuainisha vihatarishi husika pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo ili kuhakikisha malengo ya mpango na bajeti yanafikiwa kama ilivyokusudiwa.

3.2. Vihatarishi vya Mpango na Bajeti

28. Malengo ya mpango na bajeti yanaweza kuathiriwa zaidi na vihatarishi vifuatavyo;

3.2.1. Vihatarishi vya Uchumi Jumla

29. Vihatarishi vya uchumi jumla vinaweza kujitokeza kutokana na hali halisi ya mazingira ya ndani na nje ya nchi. Vihatarishi vinavyoweza kuathiri viashiria vya uchumi jumla vinatokana na matukio hatarishi ya asili na yasiyo ya asili. Pamoja na vihatarishi vingine, viashiria vya uchumi jumla huathiriwa zaidi na vihatarishi vinavyohusiana na bei za mazao, bidhaa na huduma, viwango vya riba katika soko, viwango vya kubadilisha fedha na mikopo ya sekta binafsi na sekta ya umma. Matukio, sababu na athari za vihatarishi vya uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Mabadiliko ya Bei za Bidhaa Muhimu

30. Kupanda kwa bei za bidhaa muhimu, hususan bei za bidhaa za petroli katika soko la dunia kunaweza kuathiri matumizi ya Serikali na uwezo wa wananchi kununua bidhaa na huduma. Aidha, kuyumba kwa bei za bidhaa katika soko la dunia kama vile bidhaa za madini na mazao ya biashara kutokana na mabadiliko hasi ya uchumi wa dunia na kuvurugika kwa mnyororo wa usambazaji wa bidhaa na huduma kunaweza kupunguza mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi na kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya mpango na bajeti pamoja na kuathiri thamani ya shilingi.

(ii) Kuongezeka kwa Riba za Mikopo

31. Kuongezeka kwa riba za mikopo katika masoko ya fedha ya ndani na nje ya nchi kutaathiri uwezo wa Serikali wa kukopa na kuhudumia deni lililoiva. Kuongezeka kwa gharama za mikopo katika masoko ya fedha kunaathiri mahitaji mengine ya kibajeti, hususan uagizaji wa bidhaa za mtaji na mali ghafi kwa ajili ya uwekezaji wa umma na binafsi.

(iii) Kushuka kwa thamani ya Shilingi

32. Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi la dola ya Marekani inaweza kushuka kutokana na uhaba wa fedha za kigeni nchini unaosababishwa na ongezeko kubwa la

mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kugharamia bidhaa muhimu zinazotoka nje hususan bidhaa za petroli. Kushuka kwa thamani ya shilingi kutaongeza gharama za kuhudumia deni la Serikali la nje ambalo malipo yake hufanyika kwa kutumia fedha za kigeni. Athari nyingine zinazoweza kujitokeza ni kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa bidhaa, hususan bidhaa za mitaji na malighafi kutoka nje ya nchi na hivyo kuchochea mfumuko wa bei nchini. Matokeo ya athari hizo ni ukuaji mdogo wa uchumi kutokana na gharama kubwa za uendeshaji wa biashara, uwekezaji na kupungua kwa uwezo wa wananchi kununua bidhaa na huduma na hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali.

3.2.2. Madeni Sanjari

33. Dhamana ya kukopa iliyotolewa na Serikali kwa taasisi na mashirika ya umma zinaweza kusababisha madeni, endapo taasisi na mashirika husika yatashindwa kurejesha mikopo kwa mujibu wa mikataba na hivyo kulazimu Serikali kurejesha mikopo hiyo ambayo haikuwa sehemu ya mpango na bajeti. Aidha, Serikali hulazimika kugharamia malipo ya fidia na madai yatokanayo na amri za mahakama kutokana na ukiukaji wa masharti ya mikataba. Mahitaji hayo yakijitokeza yanaweza kusababisha ongezeko la madai na deni la Serikali, kuathiri uwezo wa nchi kukopesheka, na kupunguza uwezo wa serikali kugharamia mahitaji ya kibajeti, hususan miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za kawaida.

3.2.3. Mabadiliko ya Tabianchi na Majanga ya Asili

34. Matukio ya asili kama ukame, mafuriko, mmomonyoko wa udongo, vimbunga na matetemeko ya ardhi yanasababisha uharibifu wa miundombinu, mali na vifo, kupungua kwa mapato ya taasisi, serikali na watu binafsi pamoja na uwekezaji wa sekta ya umma na binafsi. Kutokana na athari za matukio ya asili, gharama za urejeshwaji wa miundombinu, mali na misaada kwa waathirika ambayo haikuwa sehemu ya mpango na bajeti ya taasisi, serikali na watu binafsi huathiri utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa ujumla. Aidha, kwa kuzingatia kuwa kilimo kinachangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa, mabadiliko ya tabianchi yanaweza kusababisha mfumuko wa bei za chakula na kudhoofisha shughuli zinazochochea ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa bajeti ya serikali.

3.2.4. Migogoro ya Kisiasa na Mahusiano ya Kidiplomasia

35. Migogoro ya kisiasa ya ndani na nje ya nchi inaweza kuvuruga au kudumaza shughuli za kiuchumi na kijamii, na hivyo kuathiri mpango kazi wa upatikanaji wa mapato ya serikali, uwekezaji kutoka nje na mnyororo wa uhitaji na ugavi wa mazao, bidhaa na huduma ndani pamoja na mahitaji ya ziada ya ulinzi.

3.2.5. Udukuzi na Shambulio la Mifumo ya Kielektroniki

36. Mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mapato, matumizi na uendeshaji wa shughuli za Serikali inaweza kudukuliwa na kushambuliwa kutokana na vishawishi vya wizi na mazingira ya ushindani, hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali. Aidha, matumizi mabaya au udanganyifu katika matumizi ya mifumo ya

kielektroniki unaweza kuchepusha mapato na matumizi ya serikali na kudhoofisha huduma kwa jamii, hususan malipo kwa watumishi, wazabuni, huduma za kijamii na usalama wa mali na watu.

3.3. Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi

37. Ili kukabiliana na athari za vihatarishi katika utekelezaji wa mpango na bajeti, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati iliyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 3.1**:

Jedwali Na. 3.1: **Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi**

Na	Kihatarishi	Hatua ya kukabiliana na kihatarishi
1.	Vihatarishi vya uchumi jumla (i) Mabadiliko ya bei za bidhaa muhimu (ii) Kuongezeka kwa riba za mikopo (iii) Kushuka kwa thamani ya shilingi	Kuendelea kutekeleza na kusimamia sera ya fedha na bajeti kwa lengo la kuhakikisha malengo na shabaha za kiuchumi yanafikiwa.
		Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa fedha za Kigeni.
		Kuendelea kuhimiza matumizi ya nishati mbadala kama vile nishati ya gesi ili kupunguza athari za kupanda kwa bei ya bidhaa za petroli katika soko la dunia.
		Kuendelea kutenga rasilimali kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira ili kuhakikisha kilimo kinafanyika kwa vipindi vyote vya mwaka. Aidha, kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa, mbegu bora zinazohimili mabadiliko ya tabianchi, na teknolojia za kuhifadhi chakula ili kupunguza mfumuko wa bei ya chakula.
		Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Kutumia Vyanzo Mbadala ikiwemo kuhusisha sekta binafsi.
2.	Madeni sanjari	Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 kwa kutoa dhamana kwenye miradi yenye tija na kufuatilia utendaji wa mashirika kwa mujibu wa mkataba/vigezo/makubaliano ya dhamana husika
3.	Mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili	Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa 2022 - 2027 na kuimarisha Mfuko wa Taifa wa

Na	Kihatarishi	Hatua ya kukabiliana na kihatarishi
		Maafa ili kukabiliana na athari za majanga pindi yanapotokea.
		Kuendelea kutenga rasilimali kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira ili kuhakikisha kilimo kinafanyika kwa vipindi vyote vya mwaka. Aidha, kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa, mbegu bora zinazohimili mabadiliko ya tabianchi, na teknolojia za kuhifadhi chakula ili kupunguza mfumuko wa bei ya chakula
		Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032)
4.	Migogoro ya kisiasa na mahusiano ya kidiplomasia	Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa fedha za Kigeni
		Kuendelea kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo, uzalishaji wa mbolea
		Kukuza masoko ya mitaji ya ndani
5.	Udukuzi na shambulio la mifumo ya kielektroniki	Kuendelea kuimarisha usalama katika mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha za umma na shughuli za serikali
		Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma za mwaka 2023 ili kudhibiti vitendo vya udanganyifu kwa watumishi wa umma.
		Kuendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tahadhari katika taasisi zote za umma ili kubaini changamoto zinazoweza kujitokeza na kuwezesha maamuzi ya kiutendaji kufanyika kwa wakati.

4. MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

38. Sehemu hii inatoa maelekezo yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa maandalizi, uwasilishaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26. Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyorejewa katika mwongozo huu ikiwemo na mabadiliko yanayotokea baada ya Mwongozo kuidhinishwa.

4.1 Maandalizi ya Mpango na Bajeti

39. Wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia malengo na shabaha za Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/26, mipango mkakati ya kitaasisi, na maagizo mengine yaliyotolewa na Serikali. Aidha, pamoja na kuzingatia maagizo na maelekezo yaliyoainishwa katika Mipango na Mikakati, Maafisa Masuuli wanapaswa kufungamanisha vipaumbele vya Mafungu na Taasisi zake ili kufikia shabaha ya pamoja katika matokeo tarajiwa.

4.1.1 Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

40. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa Mpango na Bajeti ya Muda wa Kati (MTEF) mara baada ya Mwongozo huu kuidhinishwa. Vitabu vya MTEF viwasilishwe Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango wiki ya nne ya Januari, 2025, baada ya kuidhinishwa na Mamlaka husika. Vitabu vya MTEF kwa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma vitawasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya uchambuzi kulingana na ratiba itakayotolewa. Aidha, vitabu vya MTEF vya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa viwasilishwe Wizara ya Fedha baada ya mapitio ya Ofisi ya Rais TAMISEMI. Vilevile, randama za bajeti zitawasilishwa kwenye Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge na Uratibu. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.1**

Jedwali Na. 4.1: Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26

Mwezi	Shughuli
Agosti – Novemba 2024	Maandalizi na uidhinishwaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali
Novemba - Desemba 2024	Usambazaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na ukomo wa awali (indicative ceiling) wa bajeti za mafungu
Desemba 2024 - Februari 2025	Maandalizi ya mipango na bajeti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali; Ofisi za Wakuu wa Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi na Mashirika ya Umma
Januari - Februari 2025	Kuwasilisha na kuidhinishwa kwa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26
Januari - Mei 2025	Kufanya majadiliano kuhusu mapendekezo ya maboresho ya Mfumo wa Kodi
Februari – Machi 2025	Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango na Ofisi ya Msajili wa Hazina kufanya uchambuzi wa mipango na bajeti za kisekta na mafungu
Machi 2025	Kuwasilisha randama Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu tarehe 10 Machi kulingana na Kanuni 115 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2023
Machi 2025	Kuwasilisha kwenye Kamati ya Bunge Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26
Machi 2025	Mafungu kuwasilisha mipango na bajeti kwenye Kamati za Kisekta za Bunge
Aprili – Juni 2025	Mafungu kuwasilisha mipango na bajeti bungeni
Juni 2025	Serikali kuwasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Fedha na Sheria ya Matumizi
1 Julai 2025 - 30 Juni 2026	Utekelezaji wa mipango na bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge

4.1.2 Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya Kibajeti

41. Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kuhakikisha kuwa, uingizaji wa takwimu za bajeti kwenye mifumo ya maandalizi ya bajeti unazingatia muda uliopangwa ikiwemo masuala muhimu yafuatayo:

(i) Kufungamanisha shughuli zinazotengewa bajeti na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2020/21-2025/26 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 kwa usahihi;

(ii) Kuzingatia ukomo wa bajeti wa mwaka 2025/26 na makisio yanayoonesha uhalisia kulingana na ukomo wa miaka miwili inayofuata (2026/27 hadi 2027/28);

(iii) Kutumia kwa usahihi namba za miradi, mageresho ya kibajeti (GFS codes 2014), na vizio vya vipimo kama vilivyoainishwa kwenye mifumo;

(iv) Kuhakikisha kuwa takwimu za bajeti ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo zinazoingizwa kama *transfers* zinakasimiwa katika vifungu husika; na

(v) Kuingiza viwango sahihi vya stahili za kisheria ikiwemo posho, pango, umeme, simu na maji kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR – MUUUB).

4.1.3 Uwasilishaji wa Mpango na Bajeti (MTEF)

42. Wakati wa uwasilishaji wa mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Uwasilishaji wa MTEF uzingatie muundo uliooneshwa katika **Kiambatisho Na. 1E**;

(ii) Kuzingatia ratiba ya uwasilishaji wa mpango na bajeti kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.4.1;

(iii) Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango nakala ngumu mbili (2) za makadirio ya mapato na matumizi ya fungu husika, siku tano (5) kabla ya kuanza uchambuzi kwa kuzingatia ratiba ya uchambuzi;

(iv) Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kuwasilisha Ofisi ya Msajili wa Hazina nakala tete ya makadirio ya mapato na matumizi kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na Ofisi hiyo;

(v) Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaelekezwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi OR-TAMISEMI kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na Ofisi hiyo. Aidha, OR-TAMISEMI itawasilisha HAZINA Taarifa jumuishi ya fomu namba 3B, 4, 6 na 8B kwa mafungu yote ikiwa katika nakala tete zenye muundo wa *excel* au *access*; na

(vi) Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaelekezwa kuwasilisha Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango, OR – TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina nakala ngumu moja (1) na nakala tete zilizofanyiwa marekebisho ndani ya siku tano (5) baada ya bajeti ya fungu husika kuidhinishwa na Bunge.

4.1.4 Uwasilishaji wa Randama

43. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwasilisha randama kwa Katibu wa Bunge na nakala Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kabla au ifikapo tarehe 10 Machi, 2025 kwa mujibu wa Kanuni 115 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2023. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwasilisha randama za utekelezaji wa Mwaka 2024/25 na mpango na bajeti wa Mwaka 2025/26 kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya kamati husika itakayotolewa na Katibu wa Bunge. Muundo wa uwasilishaji wa randama ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1F.**

Tanbihi: Taarifa za ziada zitakazohitajika nje ya muundo wa randama ziwasilishwe kama kiambatisho kwenye randama.

4.2 Maelekezo ya Uandaaji wa Mpango na Bajeti

44. Sehemu hii inatoa maelekezo kuhusu Kamati za Bajeti, viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni, mkakati wa kuongeza fedha za kigeni na mapato. Maeneo mengine ni udhibiti wa uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni, uandaaji wa bajeti ya mishahara, uendeshaji wa ofisi na maendeleo.

4.2.1 Kamati za Bajeti

45. Katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha:

(i) Kamati za Bajeti zinaimarishwa na wajumbe wote kushiriki kikamilifu katika kuandaa na kutekeleza bajeti kwa mujibu wa Kifungu 18(2) na Kanuni ya 17(3) ya Sheria ya Bajeti, Sura 439;

(ii) Vikao vya Kamati za Bajeti vifanyike kwa ajili ya; kupitia mikakati ya ukusanyaji wa mapato, ugawaji wa rasilimali fedha zilizopokelewa/kukusanywa na kupitia taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti; na

(iii) Taarifa ya vikao hivyo iandaliwe kwa kuzingatia muundo uliobainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 1G** cha mwongozo huu na kuwasilishwa Wizara ya Fedha kila robo mwaka.

4.2.2 Maelekezo ya Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato

46. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa na mikakati ya kuongeza mapato na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo ya Serikali kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa yanaingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu 58(a) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo kwa mujibu wa Sheria husika;

(ii) Kuandaa, kuhuisha na kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato katika maeneo wanayosimamia kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo na kuiwasilisha Wizara ya Fedha wakati wa uchambuzi wa mpango na bajeti;

(iii) Kuwajengea uwezo viongozi na watendaji kuhusu mbinu za ukusanyaji wa mapato na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali;

(iv) Kuandaa na kuhuisha kanzidata na takwimu za vyanzo vyote vya mapato katika ngazi zote ikijumuisha kata, vijiji na mitaa kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji na udhibiti wa upotevu wa mapato kila mwaka;

(v) Kuhakikisha matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato kwa kufanya uhakiki, usuluhishi na ukaguzi wa mifumo mara kwa mara kwenye vituo vyote vya makusanyo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(vi) Kuzingatia sheria za kodi ikiwa ni pamoja na kutoza kodi ya zuio (withholding tax) na kudai risiti za kielektroniki (EFD) kwa malipo yote yanayofanywa kwa wazabuni na wakandarasi;

(vii) Kutoingia mikataba na wazabuni, wakandarasi na watoa huduma wasiotumia mashine za kielektroniki (EFD) kutoa stakabadhi;

(viii) Kuwasilisha Wizara ya Fedha kila mwezi taarifa za makusanyo kutoka kila chanzo cha mapato kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa lengo la kutathmini mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

(ix) Wizara zenye dhamana ya masuala ya biashara na uwekezaji ziratibu uanzishwaji wa dirisha la pamoja la kielektroniki la utoaji wa huduma na kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa taasisi zinazotoa huduma kwa pamoja, ili kuwezesha utoaji wa namba jumuishi kwa lengo la kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo za Serikali kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji;

(x) Kushirikisha wadau mapendekezo ya uanzishaji au mabadiliko ya viwango vya kodi, ushuru na tozo kabla ya kuwasilisha Wizara ya Fedha;

(xi) Kuanzisha na kuimarisha usimamizi wa vituo vya makusanyo hususan katika maeneo ya mipaka, viwanja vya ndege, bandari pamoja na vituo vya ukaguzi kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ili kutambua na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(xii) Kutumia fursa na changamoto zilizopo kuibua vyanzo vipya vya mapato na kutenga bajeti kwa ajili ya kuanzisha na kuwekeza katika miradi ya kimkakati ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali; na

(xiii) Kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa wakati.

4.2.3 Kiwango cha Ubadilishaji Fedha

47. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia kiwango elekezi cha ubadilishaji wa fedha za kigeni ambacho ni dola moja ya Marekani kwa shilingi za Tanzania 2,888.48 wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26.

4.2.4 Uibuaji wa Miradi Mipya

48. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuweka kipaumbele cha kukamilisha miradi inayoendelea wakati wa maandalizi ya bajeti ya 2025/26 kabla ya kuibua miradi mipya. Aidha, miradi itakayopewa kipaumbele ni ile inayochochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa za ajira.

4.2.5 Bajeti ya Mishahara

49. Wakati wa maandalizi ya ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka 2025/26, Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti ya upandishaji vyeo, ajira mpya, nyongeza ya mshahara ya mwaka, ubadilishaji kada/kazi, uhamisho na uteuzi kwa kuzingatia Mwongozo wa Uandaaji wa Ikama na Makadirio ya Bajeti ya Mishahara kwa Mwaka 2025/26 kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB);

(ii) Kuzingatia Mpango wa Rasilimaliwatu uliopo wakati wa utengaji wa bajeti ya mishahara ili kuwa na msawazo wa watumishi katika Utumishi wa Umma;

(iii) Wakala za Serikali, Taasisi, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa yanayolipa mishahara kwa makusanyo ya ndani na zinazopelekewa

fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kuhakikisha yanatenga kiwango sahihi cha michango ya kisheria ya watumishi na kuwasilisha kwa wakati katika mifuko husika ili kuepuka tozo inayotokana na ucheleweshaji wa michango hiyo na usumbufu kwa watumishi pindi wanapostaafu;

(iv) Kuandaa bajeti ya mishahara kwa kuzingatia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 3 wa Mwaka 2022 na Nyaraka za Msajili wa Hazina Na. 3, 4, 5, 6, 7, 8 na 9 za Mwaka 2022 kuhusu Marekebisho ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma na Taasisi za Serikali;

(v) Kuzingatia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2021 kuhusu Matumizi ya Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimaliwatu na Mishahara (e-Watumishi);

(vi) Bajeti ya mishahara ya ajira mpya na kupandisha vyeo watumishi wa kada za ardhi waliokuwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa itengwe na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuwa ndio Mamlaka inayosimamia watumishi hao; na

(vii) Kuzingatia gharama za marekebisho, visahihisho na nyongeza mbalimbali katika miundo ya maendeleo ya utumishi ya kada chini ya Wizara wakati wa kutenga bajeti ya mishahara na kusafisha taarifa za watumishi katika mfumo wa e-Watumishi.

4.2.6 Bajeti ya Matumizi Mengineyo

50. Wakati wa maandalizi ya makadirio ya bajeti ya matumizi mengineyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

(ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia mikakati ya kukabiliana na vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti;

(iii) Kutenga bajeti kwa kuzingatia mabadiliko ya miundo mipya ya Taasisi ikiwemo vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na Tafiti na Ubunifu;

(iv) Kutenga bajeti ya kugharamia shughuli za uendeshaji wa ofisi na kulipa stahili za kisheria kwa watumishi (posho za kujikimu, uhamisho, stahili za viongozi na likizo) ili kuepuka uzalishaji wa madeni;

(v) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi ikijumuisha bajeti ya mafunzo ya matumizi ya mifumo ya usimamizi wa fedha za umma (bajeti, ununuzi na uhasibu), upimaji utendaji kazi wa watumishi na taasisi na usimamizi wa rasilimali watu;

(vi) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi kupunguza matumizi na;

(vii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia michezo kwa watumishi.

4.2.7 Bajeti ya Maendeleo

51. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuwasilisha Wizara ya Fedha takwimu za miadi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo robo ya kwanza ya kila mwaka wa fedha ili kukamilisha maandalizi ya ukomo wa bajeti za mafungu wa mwaka unaofuata;

(ii) Kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa kwa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inajumuishwa katika bajeti ya Serikali pamoja na kupata namba ya mradi kutoka Wizara ya Fedha ili kuwezesha kuhasibiwa kwa fedha hizo;

(iii) Wizara za Kisekta ziwasilishe Wizara ya Fedha mchanganuo wa shughuli na bajeti zinazotekelezwa kwenye mafungu mengine ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kujumuishwa kwenye ukomo wa bajeti wa mafungu husika wiki ya kwanza ya Desemba, 2024;

(iv) Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2022 kuhusu uibuaji, ugharamiaji, utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo;

(v) Kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura 148 kuhusu utaratibu wa kutoa msamaha wa VAT kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo na kuwasilisha maombi ya msamaha wa kodi ya VAT kupitia mfumo wa kielektroniki;

(vi) Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 inayoelekeza kutoingia mikataba ya makubaliano na Washirika wa Maendeleo ya kupokea misaada na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha;

(vii) Kanuni ya 5(b) ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 inayoelekeza kuwa mikataba yote ya mikopo itakayosainiwa inapaswa kuzingatia miradi ya kimkakati inayozalisha mapato (investment projects) na maeneo ya vipaumbele;

(viii) Kutenga mchango wa Serikali (counterpart fund) katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo;

(ix) Kukamilisha taratibu zote za maandalizi ya mradi ikiwemo upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za mazingira na jamii kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi;

(x) Kutenga bajeti ya kugharamia fidia katika maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi;

(xi) Kutumia njia mbadala kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo (Alternative Project Financing - hati fungani, mikopo na PPP) yenye mlengo wa kibiashara kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizopo;

(xii) Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 iliyoweka ukomo wa zabuni zinazoweza kutolewa kwa wasio wazawa ili kuwawezesha wazawa (local content) na kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi;

(xiii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti na maendeleo kwa kutumia mapato ya ndani ya taasisi na ruzuku kutoka Serikali Kuu;

(xiv) Kutenga bajeti kwa ajili ya upimaji na upatikanaji wa hati miliki ya maeneo yanayomilikiwa na taasisi za umma;

(xv) Kuzingatia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na masuala ya jamii katika upangaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo;

(xvi) Kujenga uwezo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi, Mashirika ya Umma, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu dhana ya PPP;
(xvii) Kuzingatia matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS); na
(xviii) Ushirikishaji wa sekta husika katika utekelezaji wa miradi inayohusisha sekta zaidi ya moja kabla, wakati na baada ya utekelezaji.

4.2.8 Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni

52. Katika kutekeleza mkakati wa kuongeza fedha za kigeni kwa kuzingatia Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea:

(i) Kusimamia utekelezaji wa kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu, Sura 197, na Sheria ya Fedha za Kigeni, Sura 271 na Kanuni zake kwa lengo la kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni;
(ii) Kutekeleza Mikakati ya Wizara ya Kukabiliana na Uhaba wa Fedha za Kigeni inayobainisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuimarisha akiba ya fedha za kigeni;
(iii) Kuhakikisha mikataba ya ndani mipya inayoingiwa inatumia shilingi ya Tanzania kwa lengo la kupunguza uhitaji wa matumizi ya fedha za kigeni yasiyo ya lazima. Pia, kuhakikisha mikataba ya zamani iliyoingiwa kwa fedha za kigeni inafanyiwa mapitio;
(iv) Kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa mauzo ya nje;
(v) Kuimarisha uzalishaji wa bidhaa na huduma mbadala ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni;
(vi) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia mitaji kutoka nje ya nchi ikiwemo watanzania waliopo nje ya nchi kuwekeza na kutuma fedha za kigeni; na
(vii) Kusimamia utekelezaji wa kifungu cha 60 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 inayoagiza kutoa kipaumbele kwa bidhaa na huduma za ndani ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, kuimarisha soko la ndani, kulinda viwanda vya ndani na kuongeza ajira.

4.2.9 Mikakati ya Ulipaji na Udhibiti wa Ulimbikizaji wa Madeni

53. Katika kudhibiti uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia:

(i) Kifungu cha 52 (1-2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 kinachohusu mfumo wa udhibiti wa miadi;
(ii) Maelekezo ya *Treasury Circular No. 2 of 2022/23 on Government Domestic Expenditure Arrears and Other Outstanding Obligations* kwa lengo la kuendelea kusimamia na kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti na Kuzuia Malimbikizo ya Madeni;
(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia ulipaji wa madeni kwa kuzingatia miongozo na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348;

(iv) Ulipaji wa madeni uzingatie umri wa madeni pamoja na kutoa kipaumbele kwenye madeni yenye riba na adhabu; na

(v) Kuhakikisha madai yanayotokana na bidhaa au huduma katika mwaka wa utekelezaji wa bajeti yanalipwa kwa wakati na kiasi stahiki kwa kutumia fedha za migao/makusanyo ya kila mwezi ili kuepuka uzalishaji wa madeni.

4.2.10 Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

54. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kusimamia nidhamu na uwajibikaji kwa matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kuwa fedha zote zinazopokelewa/zinazokusanywa zinatumika kwa wakati kwa mujibu wa mpango kazi ili kuepuka fedha hizo kuvuka mwaka wa fedha husika;

(ii) Kutekeleza Mwongozo wa Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali wa mwaka 2021 unaosisitiza kutoingia mikataba bila kuwa na bajeti ya shughuli husika;

(iii) Kuhakikisha ushirikishwaji wa taasisi za kisekta unazingatiwa wakati wa upangaji na utekelezaji wa miradi;

(iv) Kuimarisha utendaji wa Kamati za Bajeti, vitengo vya ukaguzi wa ndani pamoja na ufuatiliaji na tathmini ili kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwemo miradi inayotekelezwa kwa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; na

(v) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (National e-Procurement System of Tanzania - NeST) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi pamoja na kuzingatia bei ya soko wakati wa ununuzi.

4.3 Maelekezo Mahsusi kwa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma

55. Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kuhakikisha mifuko ya hifadhi ya jamii inakuwa na taarifa sahihi za wanachama ili kuondoa usumbufu wakati wa kustaafu au kumaliza mikataba ya kazi;

(ii) Kuhakikisha taasisi za kibiashara na za kimkakati zinazingatia Waraka wa Msajili wa Hazina Na.1 wa mwaka 2023, katika kuimarisha mfumo wa usimamizi na utendaji kazi;

(iii) Kuhakikisha taasisi zinatenga michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa kuzingatia kifungu cha 8(1)(f) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura 370;

(iv) Kuwasilisha asilimia 70 ya ziada ya mapato katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa kuzingatia kifungu cha 10(2) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura 370;

(v) Kuhakikisha maombi ya kuvuka mwaka na fedha yanawasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina na zinatumika kwa malengo yaliyopangwa awali kulingana na sheria na kanuni. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina inapaswa kuwasilisha Wizara ya Fedha maombi ya kuvuka mwaka na fedha kwa kuzingatia kifungu cha 29 (2-3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439;

(vi) Kuhakikisha maombi ya uhamisho wa bajeti yanawasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili awasilishe Wizara ya Fedha kwa kuzingatia Kifungu cha 28 (1-4) cha Kanuni za Sheria ya Bajeti, Sura 439;
(vii) Kuhakikisha taasisi zinazodaiwa na taasisi nyingine za umma zinatenga bajeti na kulipa madeni hayo kwa wakati;
(viii) Kuandaa na kuwasilisha Ofisi ya Msajili wa Hazina mikakati ya kuongeza mapato katika maeneo wanayosimamia kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo;
(ix) Kuzingatia maelekezo ya Katibu Mkuu OR-MUUUB kuhusu siku za likizo na malipo ya nauli ya likizo yaliyotolewa kwa barua yenye Kumb. Na. CAC.17/228/01/07 ya tarehe 09 Novemba, 2023.

4.4 Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

56. Sehemu hii inatoa maelekezo yanayopaswa kufuatwa na Maafisa Masuuli wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/26.

4.4.1 Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa

57. Wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/26, Maafisa Masuuli wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kusimamia na kudumisha masuala ya usalama ikiwemo kugharamia vikao vya Kamati za Usalama ngazi ya Mkoa, Wilaya na Vikao vya Kisheria katika Tarafa;
(ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati, ukamilishaji na ujenzi wa ofisi na makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa;
(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuhuisha Wasifu wa Uwekezaji na kufanya makongamano ya uwekezaji;
(iv) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kutoa taarifa kila nusu mwaka na kwa mwaka kwa OR-TAMISEMI;
(v) Kutenga bajeti kwa ajili ya kujikinga dhidi ya majanga pamoja na maafa mbalimbali ikiwemo moto, mafuriko na mlipuko wa magonjwa;
(vi) Kuandaa Mipango ya Hifadhi ya Mazingira (Local Environmental Action Plans) kulingana na changamoto za Mazingira katika mikoa na kuhakikisha fedha zinatengwa kwa ajili utekelezaji wa Mipango hiyo;
(vii) Kutumia mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathimini (Intergrated Monitoring and Evaluation System- iMES) katika shughuli za miradi ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;
(viii) Kusimamia utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kupitia mwongozo mpya wa mwaka 2024 kwa vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; na
(ix) Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Wajibu wa Makampuni katika Jamii (Corporate Social Responsibility- CSR).

4.4.2 Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

58. Wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/26, Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuandaa na kujumuisha kwenye Mpango na Bajeti makadirio ya mapato na matumizi ya Kata, Vijiji/Mitaa na vituo vya kutolea huduma;

(ii) Kutenga bajeti ya miundombinu wezeshi kwa ajili ya matumizi ya Serikali Mtandao na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo hususan maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi;

(iv) Kutenga na kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wajasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kutumia mwongozo wa mwaka 2024;

(v) Kutenga bajeti kwa ajili ya miradi ya kimkakati inayogusa mawanda mapana ya wananchi kwa halmashauri zinazochangia asilimia 70, 60 na 40 ya fedha za maendeleo kwa mapato ya ndani;

(vi) Kutenga bajeti kwa ajili ya kupima maeneo ya taasisi zilizopo katika Halmashauri ambazo ni pamoja na shule, vituo vya kutolea huduma za afya, ofisi za halmashauri, kata, vijiji/mitaa na vitongoji;

(vii) Kwa kuzingatia ufinyu wa ardhi katika Halmashauri za majiji, manispaa na miji, utengaji wa bajeti ya ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa miundombinu ya elimu, afya na vitega uchumi uzingatie muundo wa ujenzi wa ghorofa;

(viii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwatambua, kuwasajili na kuwapanga wafanyabiashara wadogo (wamachinga) katika maeneo maalumu ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kufanyia biashara;

(ix) Kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa fidia maeneo yaliyotwaliwa na yatakayotwaliwa na halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umma;

(x) Kuandaa Mipango ya Hifadhi ya Mazingira (Local Environmental Action Plans) kwa kuzingatia changamoto za Mazingira katika Halmashauri husika na kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji;

(xi) Kutenga bajeti ya kulipa madeni ya watumishi, wazabuni na wakandarasi;

(xii) Halmashauri zinazodaiwa fedha za mkopo wa mradi wa kupima, kupanga na kumilikisha ardhi zinapaswa kutenga fedha kwa ajili ya kurejesha mkopo huo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

(xiii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa miradi ya kuzalisha mapato kabla ya kuanza utekelezaji;

(xiv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kufanya msawazo wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xv) Kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa majengo ya utawala ya Ofisi za Halmashauri, Kata na Vijiji/Mitaa;

(xvi) Kutenga kiasi kisichopungua shilingi 200,000 kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi kwa kila Kata, Kijiji/Mtaa kila robo mwaka. Aidha, kwa Halmashauri zinazokusanya mapato chini ya shilingi bilioni

1.5 zinaelekezwa kutenga kiasi kisichopungua shilingi 100,000 kwa Kata, Kijiji/Mtaa kila robo mwaka;

(xvii) Kuendelea kutenga shilingi 100,000 kila mwezi kwa ajili ya posho ya madaraka ya watendaji wa kata;

(xviii) Kutenga na kurejesha bajeti ya mapato yatokanayo na mazao ya kilimo (asilimia 20), mifugo (asilimia 15) na uvuvi (asilimia 5) ili kuboresha na kuendeleza sekta hizo;

(xix) Kufunga Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Tanzania (Centralized GoT – HoMIS) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika vituo ambavyo bado havijafunga mfumo huo;

(xx) Kutenga bajeti kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuchangia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 290;

(xxi) Halmashauri ambazo zimepata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kutenga bajeti kutoka kwenye mapato yao ya ndani kwa ajili ya marejesho ya mkopo;

(xxii) Mwongozo wa Uanzishaji na Usimamizi wa Kampuni Mahsusi za Uendeshaji wa Miradi ya Vitega Uchumi kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(xxiii) Kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za ustawi wa jamii;

(xxiv) Kusimamia na kutekeleza uandaaji wa Mpango wa Wajibu wa Makampuni katika Jamii (Corporate Social Responsibility- CSR);

(xxv) Kutambua na kurasimisha shughuli za kiuchumi zisizo rasmi ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato;

(xxvi) Kutenga bajeti kwa ajili ya uhamasishaji wa matumizi ya huduma ndogo za fedha ili kuwezesha wananchi kutumia huduma rasmi za fedha;

(xxvii) Kutenga bajeti za matengenezo na mafuta ya vyombo vya usafiri kwa Watendaji wa Kata ili kuwezesha ufuatiliaji wa shughuli za ukusanyaji na usimamizi wa mapato na mikopo ya asilimia 10;

(xxviii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kamati za ushauri wa kisheria na kamati ya msaada wa kisheria ya Mkoa; na

(xxix) Kuendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia madaraja ya Halmashauri kwa mujibu wa maelekezo ya Katibu Mkuu OR-TAMISEMI yaliyotolewa kwa barua yenye Kumb. Na. CFC.133/307/01/157 ya tarehe 12 Desemba, 2022. Mgawanyo wa madaraja ni kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na.4.2**.

Jedwali Na.4.2 : Mgawanyo wa Mapato ya Ndani kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Na	Daraja la Halmashauri	Kiwango cha Mapato yasiyolindwa	Asilimia ya Kuchangia kwenye miradi	Asilimia ya fedha za miradi - kuchangia mikopo ya Vikundi	Asilimia ya fedha za miradi - kuchangia TARURA	Asilimia ya kuchangia miradi mingine
1	Daraja la Kwanza	Bilioni 20 au zaidi	70	10	10	50
2	Daraja la Pili	Bilioni 5 au zaidi	60	10	10	40
3	Daraja la Tatu	Bilioni 2 hadi 5	40	10	-	30
4	Daraja la Nne	Chini ya Bilioni 2	20	10	-	10

Chanzo: OR - TAMISEMI

4.4.3 Maelekezo ya Kisekta katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Shule za Msingi na Sekondari kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023;

(ii) Kuandaa na kuwasilisha takwimu OR-TAMISEMI kwa ajili ya kuwezesha utengaji wa bajeti ya Elimumsingi na Sekondari (Kidato cha V na VI) ifikapo tarehe 31 Desemba, 2024;

(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na chanjo pamoja na kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano ili kuimarisha huduma za lishe;

(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga, kukamilisha na kukarabati miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za jamii;

(v) Kutenga bajeti ya uhamasishaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi kushiriki katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na sekta husika;

(vi) Kuendelea kutenga bajeti za matengenezo na mafuta ya vyombo vya usafiri kwa Maafisa Ugani na Watendaji wa Kata ili kuwezesha ufuatiliaji wa shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na shughuli nyingine za Serikali katika Kata;

(vii) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za kiuchumi;

(viii) Kuendeleza mipango miji na kufanya matumizi bora ya ardhi katika vijiji, kuendeleza miji midogo inayochipukia pamoja na kurasimisha makazi yaliyojengwa kiholela;

(ix) Kutenga bajeti kwa ajili ya kamati za ushauri wa kisheria na kamati ya maadili ya wilaya ya mahakama; na

(x) Kutenga bajeti ya usimamizi na uendelezaji wa maliasili, malikale na mazingira.

4.5 Masuala Mengine Muhimu ya Kuzingatiwa Wakati wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti

59. Pamoja na maelekezo ya ujumla na mahsusi yaliyotolewa, masuala mengine muhimu yanayopaswa kuzingatiwa ni: Masuala ya muungano; ushirikiano wa kikanda na kimataifa; Ujenzi wa Mji wa Serikali na Taasisi za Umma Jijini Dodoma; Uchumi wa Buluu; Uchumi wa kidigitali; masuala ya watu wenye ulemavu; masuala ya kijinsia; mazingira; afua za lishe; VVU, UKIMWI, afya ya akili na magonjwa sugu yasiyoambukiza; mapambano dhidi ya rushwa; mapambano dhidi ya dawa za kulevya; uwekezaji wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; uwezeshaji wananchi kiuchumi; masuala ya haki jinai pamoja na masuala ya Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma.

4.5.1 Masuala ya Muungano

60. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa:

(i) Kuhakikisha kuwa hoja za muungano zinaendelea kushughulikiwa; na

(ii) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha shughuli za ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

4.5.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

61. Katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework* - DCF) wa mwaka 2017/18 - 2024/25 pamoja na mpango kazi wake;

(ii) Kuendelea kuzingatia itifaki, mikataba na makubaliano baina ya Tanzania na nchi nyingine na ile ya kikanda na kimataifa inayojumuisha Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mashirika ya Kimataifa;

(iii) Kuwasilisha Wizara ya Fedha makadirio ya michango ya uanachama wa kikanda na kimataifa ndani ya wiki ya kwanza ya Desemba, 2024 kwa ajili ya kujumuishwa kwenye bajeti;

(iv) Kuendelea kutumia kikamilifu fursa zilizopo katika makubaliano kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa manufaa ya Taifa kwa kuzingatia diplomasia ya uchumi; na

(v) Kutenga bajeti ya kugharamia utekelezaji wa viashiria vilivyoainishwa na washirika wa maendeleo kama vigezo vya kuipatia nchi msaada wa kibajeti ili kuiwezesha nchi kukidhi vigezo vya kupata fedha.

4.5.3 Ujenzi wa Miundombinu na Ofisi za Wizara na Taasisi za Umma Katika Mji wa Serikali Jijini Dodoma

62. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia mahitaji ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu na ofisi za Wizara na Taasisi katika Mji wa Serikali na Makao Makuu

Dodoma. Hii ni pamoja na kuzingatia madai ya wakandarasi na washauri elekezi pamoja na gharama za samani ili kuhakikisha ujenzi wa awamu ya pili unakamilika kabla ya kuanza awamu nyingine.

4.5.4 Uchumi wa Buluu

63. Maafisa Masuuli wa sekta zinazoguswa na uchumi wa buluu wanaelekezwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 ili kuibua na kutumia fursa zitokanazo na rasilimali za maji bahari na baridi kwa lengo la kukuza uchumi na kuchochea maendeleo ya Taifa.

4.5.5 Uchumi wa Kidigitali

64. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidigitali 2024–2034 kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga mfumo jumuishi wa kisekta na kuhakikisha mfumo huo unabadilishana taarifa na mifumo mingine;
(ii) Kuhakikisha mifumo inayotoa huduma kwa wananchi inaunganishwa na mfumo wa utambuzi wa watu (Jamii Namba);
(iii) Kuhakikisha vituo vya kutolea huduma kwa wananchi vinaunganishwa na mtandao wa intaneti ili kuboresha utoaji wa huduma; na
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuandaa miongozo ya matumizi ya TEHAMA kwa sekta.

4.5.6 Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

65. Katika eneo hili Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010 hususan kwa;

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu wezeshi katika vituo vyote vya kutolea huduma kwa ajili ya watu wenye ulemavu;
(ii) Kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu Tanzania wa Mwaka 2022;
(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu; na
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya mahitaji ya watumishi wa umma wenye ulemavu kwa kuzingatia Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu wa Mwaka 2008.

4.5.7 Uandaaji wa Bajeti yenye Mlengo wa Kijinsia

66. Katika uandaaji wa bajeti yenye mlengo wa kijinsia (gender responsive budgeting), Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutambua masuala ya kijinsia katika maeneo yao kwa kufanya uchambuzi wa takwimu ili kutekeleza hatua za kukabiliana na upungufu uliobainika katika taasisi husika;
(ii) Kutekeleza Mpangokazi wa Pili wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II 2024/25 – 2028/29);

(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha miundombinu inayozingatia jinsia; na
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya mafunzo kuhusu uandaaji wa mipango na bajeti yenye mlengo wa kijinsia.

4.5.8 Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

67. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi katika uandaaji na utekelezaji wa mipango na bajeti ikiwa ni pamoja na:

(i) Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) ili kupunguza uharibifu wa mazingira, changamoto za mabadiliko ya tabianchi na kupunguza vifo vinavyotokana na matumizi ya nishati isiyo safi (hatarishi);
(ii) Kutoa elimu na kutekeleza Mwongozo wa Biashara ya Kaboni wa Mwaka 2022 ili kuiongezea mapato jamii na Serikali;
(iii) Kuibua miradi ambayo inaweza kupata fedha kutoka kwenye mifuko ya kimataifa inayosaidia nchi zinazoendelea katika kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na uhifadhi wa mazingira;
(iv) Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032);
(v) Kujumuisha masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira wakati wa maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti ili kuongeza uwezo wa nchi kuzuia, kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;
(vi) Kutenga bajeti kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja kujipanga na kutathmini majanga ya asili yanayoweza kutokea;
(vii) Kufuatilia vyanzo vya mapato vinavyotokana na masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha fedha hizo zinaelekezwa kushughulika masuala ya mabadiliko ya tabianchi na shughuli za maendeleo;
(viii) Kuhakikisha taarifa za mapato na matumizi ya fedha zinazotokana na mazingira na mabadiliko ya tabianchi zinajumuishwa kwenye taarifa za utekelezaji; na
(ix) Kuhakikisha mpango wa maendeleo na bajeti ya Taifa inahusisha jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kufungamanisha na usawa wa kijinsia ipasavyo.

4.5.9 Afua za Lishe

68. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia utekelezaji wa Mpango wa Pili Jumuishi wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (NMNAP – II) wa Mwaka 2021/22 – 2025/26 ili kukabiliana na changamoto ya lishe duni kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi sahihi ya chakula yanayoendana na lishe;
(ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa huduma za lishe bora ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za jamii;
(iii) Kutenga bajeti ya kuimarisha ushirikishaji wa sekta mbalimbali na sekta binafsi katika masuala ya lishe;

(iv) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya afua za lishe kupitia *Objective Y*; na
(v) Kuhakikisha fedha za lishe zinatumika kama zilivyokusudiwa.

4.5.10 VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza

69. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:
(i) Kuendelea kutekeleza matakwa ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa VVU na UKIMWI, Sura 431;
(ii) Kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya Mwaka 2001 na Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania 2021/22 - 2025/26 (NMSF - V);
(iii) Kutenga bajeti na kuzingatia maelekezo ya Mwongozo na Waraka Na. 2 wa Utumishi wa Umma wa Mwaka 2014 kuhusu kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma; na
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza afua za kudhibiti magonjwa ya afya ya akili kwa watumishi wa umma.

4.5.11 Mapambano Dhidi ya Rushwa

70. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya afua za kupambana na rushwa na kuzingatia Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne 2023/24-2029/30 kwa mujibu wa Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2024

4.5.12 Mapambano Dhidi ya Dawa za kulevya

71. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea kuzingatia Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura 95 na maelekezo ya Mwongozo wa Utoaji Elimu Kuhusu Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini wa Mwaka 2022.

4.5.13 Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

72. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103, Sheria ya Bajeti, Sura 439, Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2022 na Waraka Na. 7 wa Hazina wa Mwaka 2021 kuhusu miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa PPP. Aidha, maafisa masuuli wanaelekezwa kuibua na kuanisha miradi inayoweza kutekelezwa na sekta binafsi.

4.5.14 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

73. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004, Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wa Mwaka 2013 na mwongozo wake pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi ya kiuchumi ili kuwezesha wananchi kutumia kikamilifu fursa zinazopatikana katika maeneo yao hususan sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, nishati, madini, biashara, masoko, michezo na huduma za kifedha. Aidha, Maafisa

Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Kifungu cha 35 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kuhusu upendeleo wa kipekee kwa makundi maalumu.

4.5.15 Masuala ya Haki Jinai

74. Maafisa Masuuli wanaohusika katika mnyororo wa Haki Jinai wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai/Mkakati wa Haki Jinai kwa kuzingatia yafuatayo: -

(i) Kuwajengea uwezo watumishi wa taasisi za Haki Jinai ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi;
(ii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wa mwananchi katika mnyororo mzima wa Haki Jinai kwa ajili ya ustawi wa utawala bora nchini;
(iii) Kutoa mrejesho kwa umma kuhusu mafanikio yanayotokana na utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai;
(iv) Kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai;
(v) Kuratibu na kusimamia mchakato wa marekebisho ya sheria zinazotumika kwenye Haki Jinai ambazo utekelezaji wake unaleta changamoto kwenye baadhi ya maeneo;
(vi) Kuratibu uanzishwaji wa Mfumo Jumuishi wa Haki Jinai utakaounganisha taasisi zote za Haki Jinai utakaosaidia katika kubadilishana taarifa za kiuhalifu na zinazohusiana na hizo;
(vii) Kutekeleza programu za maboresho zilizoandaliwa kwa ajili ya kuboresha utendaji wa taasisi za Haki Jinai na mfumo wa utoaji haki nchini;
(viii) Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa huduma bora kwa watu wenye mahitaji maalum kwenye taasisi za Haki Jinai; na
(ix) Kuimarisha mfumo wa uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai.

4.6 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

75. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Mwongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mwaka 2024 pamoja na masuala yafuatayo wakati wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti:

4.6.1 Ufuatiliaji na Tathmini

76. Ili kuboresha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kutenga bajeti ya kuimarisha utendaji kazi wa vitengo vipya vya ufuatiliaji na tathmini na kuwajengea uwezo wataalam wa ufuatiliaji na tathmini pamoja na kurithisha maarifa kwa watumishi wapya;
(ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera, mipango mikakati pamoja na malengo ya taasisi ili kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za taasisi kwa kuzingatia ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025;

(iii) Kuhakikisha Kamati ya Bajeti inapitia na kujadili taarifa za ufuatiliaji, tathmini na utekelezaji kila robo mwaka ili kuleta uwajibikaji;
(iv) Kuendelea kuandaa mpango na bajeti wa taasisi unaoakisi malengo, shabaha na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; na
(v) Kuimarisha mifumo ya uandaaji na utunzaji wa takwimu za utekelezaji wa shughuli za taasisi.

4.6.2 Uandaaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti

77. Maafisa Masuuli wanapaswa kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka ndani ya siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka husika kwa mujibu wa Kifungu cha 55 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake. Aidha, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji za mwaka Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango kabla ya tarehe 15 Oktoba. Nakala za taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwasilishwe OR – TAMISEMI, Taasisi na Mashirika ya Umma ziwasilishwe Ofisi ya Msajili wa Hazina na nakala kwa Wizara mama.

4.7 Maelekezo kuhusu Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu

78. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufanya maandalizi stahiki kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2025 kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2024 pamoja na maelekezo mahsusi yatakayotolewa na Serikali.

KIAMBATISHO NA. 1

VIAMBATISHO VYA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26

YALIYOMO

Kiambatisho Na. 1A **..... 1**

MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI..... 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi 1

1.3 Deni la Serikali 7

Kiambatisho Na. 1B **..... 9**

MPANGO KAZI WA KUKABILIANA NA VIHATARISHI..... 9

Kiambatisho Na. 1C **..... 12**

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24..... 12

2.1 Utangulizi 12

2.2 Mapato na Matumizi 12

2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24.... 13

2.4 Fursa zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti..... 28

2.5 Changamoto Zilizojitokeza katika Utekelezaji wa Bajeti 29

2.6 Hatua za Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti 30

2.7 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25 31

Kiambatisho Na. 1D **..... 33**

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25 33

3.1 Utangulizi 33

3.2 Sura ya Bajeti ya Mwaka 2024/25 33

3.3 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25..... 34

Kiambatisho Na. 1E **..... 42**

MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2025/26 - 2027/28 42

Kiambatisho Na. 1F**..... 44**

RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26. 44

Kiambatisho Na. 1G **..... 48**

MUUNDO WA TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI..... 48

Kiambatisho Na. 1A

MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

1.1 Utangulizi

1. Kiambatisho hiki kinaelezea mwenendo wa hali ya uchumi wa dunia, kikanda na Tanzania kwa mwaka 2023 na mwelekeo wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2024 hadi mwaka 2025 pamoja na deni la Serikali.

1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi

1.2.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Kikanda

2. Uchumi wa dunia umeendelea kukua licha ya kukabiliana na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika nchi zilizoendelea, migogoro ya kikanda, kuongezeka kwa bei za bidhaa za petroli, gharama kubwa za mikopo na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF *World Economic Outlook* (WEO), toleo la Julai 2024, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2022. Ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2024 na asilimia 3.3 mwaka 2025. Katika nchi zilizoendelea, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2022. Uchumi wa nchi zilizoendelea unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 na asilimia 1.8 mwaka 2025. Uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea ulikua kwa wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2024 na 2025.

3. Uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikua kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2024 na asilimia 4.1 mwaka 2025. Uchumi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ulikua kwa wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.7 na asilimia 3.9 mwaka 2024 na 2025, mtawalia. Kwa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2022. Kwa mwaka 2024, uchumi unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.4 na asilimia 6.1 mwaka 2025.

Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia na Kikanda (Asilimia)



1.2.2 Ukuaji wa uchumi wa Tanzania

4. Shughuli za kiuchumi zimeendelea kuimarika licha ya kukabiliana na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika nchi zilizoendelea, migogoro ya kikanda, kuongezeka kwa bei za bidhaa za petroli, gharama kubwa za mikopo na mabadiliko ya tabianchi. Pato halisi la Taifa lilifikia shilingi bilioni 148,399.76 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 141,247.19 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 5.1 ikilinganishwa asilimia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kilimo, ujenzi na uchimbaji madini. Viashiria vya kiuchumi katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024 vinaonesha uchumi kuendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazoendelea za kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, Pato halisi la Taifa kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2024, lilikua kwa wastani wa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Vilevile, Pato halisi la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2025. Ukuaji huu utategemea utekelezaji endelevu wa miradi mikubwa ya kimkakati inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji, jitihada za Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji, utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili – ASDP II, pamoja na uwekezaji wa Serikali katika sekta za huduma za kijamii.

Kielelezo Na. 1.2: Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania (Asilimia)



5. Mwaka 2023, shughuli zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa ni Kilimo (asilimia 26.5), ujenzi (asilimia 13.2), madini (asimilia 9.0), biashara (asilimia 8.3), usafirishaji (asilimia 7.2) na viwanda (asilimia 7.0) kama ilivyoainishwa kwenye Kielelezo Na. 1.3.

Kielelezo Na. 1.3: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa, Mwaka 2023 (Asilimia)



1.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia na Kikanda

6. Mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi kutokana na utekelezaji wa sera za fedha zinazopunguza ukwasi katika uchumi. Mfumuko wa bei wa dunia unatarajiwa kushuka kutoka wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2023 hadi asilimia 5.9 mwaka 2024 na asilimia 4.4 mwaka 2025[1]. Mwenendo wa mfumuko wa bei katika nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC umeonekana kuwa ndani ya wigo wa wastani wa asilimia 8 kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ongezeko la ukwasi pamoja na kupungua kwa bei za vyakula na nishati.

[1] *IMF World Economic Outlook* – WEO, toleo la Julai 2024

1.2.4 Mfumuko wa Bei Tanzania

7. Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.2 mwaka 2023/24, kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la nchi na mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC), na chini ya asilimia 4.7 mwaka 2022/23. Kupungua huko kulisababishwa na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha, kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi na utoshelevu wa chakula nchini. Aidha, mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la nchi la asilimia 3 - 5, ukichangiwa na matarajio ya upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, kuimarika kwa upatikanaji wa umeme hususan kutokana na kukamilika kwa mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere, kuimarika kwa miundombinu ya usafirishaji, utulivu wa bei za bidhaa katika soko la dunia pamoja na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti.

Kielelezo Na. 1.4: Mfumuko wa Bei Tanzania (Asilimia)



1.2.5 Utekelezaji wa Sera ya Fedha

8. Matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha yalikuwa ya kuridhisha licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali, hususan zilizotokana na mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia. Aidha, Januari 2024, Benki Kuu ilianza rasmi kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate - CBR), lengo likiwa ni kuongeza ufanisi wa sera ya fedha ili kuendana na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi. Kupitia mfumo huu, Benki Kuu ya Tanzania itakuwa inatoa mwelekeo wa riba itakayotumika katika soko la fedha baina ya mabenki. Riba ya Benki Kuu italenga kuwezesha ukwasi katika uchumi unaoendana na malengo ya kudhibiti mfumuko wa bei na kuwezesha ukuaji wa uchumi. Kwa muktadha huu, mabadiliko ya Riba ya Benki Kuu yatakuwa yanaashiria mwelekeo wa sera ya fedha katika kipindi husika. Riba hiyo pia itatumika kama kiashiria kimojawapo katika upangaji wa riba zinazotozwa na mabenki na taasisi nyingine za fedha nchini[2].

[2] https://www.bot.go.tz/Adverts/PressRelease/sw/2024010314181718.pdf

9. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa imara, licha ya kasi ya ukuaji kupungua. Mikopo kwa sekta binafsi ilifikia shilingi bilioni 34,980.85 mwezi Juni 2024 kutoka shilingi bilioni 29,835.56 Juni 2023, sawa na ongezeko la asilimia 17.2. Mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa zaidi kwenye kilimo, uchimbaji madini, uchukuzi na mawasiliano, shughuli binafsi, na uzalishaji viwandani.

Kielelezo Na. 1.5: Sehemu ya mikopo kwa jumla ya mikopo



Kielelezo Na. 1.6: Mchango wa shughuli za uchumi katika ukuaji wa mikopo



1.2.6 Viwango vya Riba

10. Riba za dhamana za Serikali ziliongezeka hadi wastani wa asilimia 9.14 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 5.73 mwaka 2022/23. Aidha, riba za mikopo zilipungua hadi wastani wa asilimia 15.47 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 16.04 mwaka 2022/23. Riba za amana ziliongezeka kidogo hadi asilimia 7.32 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 7.16 kwa mwaka 2022/23. Riba za mikopo zinatarajiwa kupungua kutokana na hatua zinazochukuliwa na Benki Kuu katika kuimarisha soko la fedha.

1.2.7 Viwango vya Ubadilishaji Fedha

11. Katika mwaka 2023/24, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kwa wastani wa asilimia 8.5 ikilinganishwa na takriban asilimia moja kwa mwaka 2022/23. Kupungua huko kulitokana na uamuzi wa benki kuu za nchi zilizoendelea kupandisha riba ili kukabiliana na mfumuko wa bei pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, hususan bidhaa za petroli kulikosababisha ongezeko kubwa la mahitaji ya fedha za kigeni. Thamani ya shilingi inatarajiwa kuimarika kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni ikiwemo katazo la matumizi ya fedha za kigeni katika kufanya malipo nchini na kuongeza uzalishaji ili kukidhi soko la ndani na kuuza nje.

1.2.8 Akiba ya Fedha za Kigeni

12. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi Juni 2024, akiba ya

fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,345.51, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.4. Kiwango hiki kimekidhi takwa la kisheria la uwepo wa akiba ya fedha za kigeni inayokidhi lengo la nchi la miezi 4.0 ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi.

1.2.9 Sekta ya Fedha

a) Huduma Jumuishi za Fedha

13. Katika kutekeleza Mpango Mkakati wa Huduma Jumuishi za Kifedha (2023 – 2028), Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya malipo ya kielektroniki na kuwezesha matumizi ya simu za mkononi katika huduma za kifedha hatua zinazolenga kuongeza muingiliano baina ya watoa huduma za fedha nchini. Aidha, ili kuimarisha huduma jumuishi za fedha, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya fedha kwa kutoa elimu na kufanya tafiti kuhusu hali ya huduma za kifedha nchini.

b) Huduma Ndogo za Fedha

14. Ukuaji wa huduma ndogo za fedha nchini umeendelea kuimarika katika kipindi cha muda wa kati. Huduma hizi, ambazo ni sehemu ya huduma jumuishi za fedha, zinahusisha mikopo midogo, bima ndogo (microinsurance) na huduma nyingine za kifedha ambazo zinaweza kupatikana kupitia uanzishaji na uendelezaji wa vikundi vya kijamii vya huduma za fedha - Community Microfinance Groups. Hadi Juni 2024, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa leseni 1,951 kwa watoa huduma daraja la pili na leseni 937 kwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo pamoja na kusajili vikundi 53,448 vya kijamii. Aidha, watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili wamekopesha mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 718.13 mwaka 2023/24 kwa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini.

c) Ukwasi na Faida katika Benki za Biashara

15. Benki za biashara zimeendelea kuimarika na kutengeneza faida zikiwa na viwango vya kutosha vya mitaji na ukwasi. Kwa mwaka 2023/24, faida baada ya kodi ilikuwa shilingi bilioni 1,060.87 kutoka shilingi bilioni 727.10 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 45.9. Taasisi za benki zimeendelea kutumia TEHAMA katika kutoa huduma za kifedha nchini, na hivyo kuongeza amana na rasilimali. Uwiano wa mtaji kwa rasilimali zote ulifikia asilimia 19.3 Juni 2024, ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika kisheria cha asilimia 10.

d) Mikopo Chechefu

16. Ubora wa rasilimali za benki uliendelea kuongezeka ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua hadi asilimia 4.1 Juni 2024 kutoka asilimia 5.3 Juni 2023. Kupungua kwa mikopo chechefu kunatarajiwa kuchagiza ongezeko la

mikopo kwa sekta binafsi pamoja na kupungua kwa riba za mikopo. Aidha, katika kudhibiti mikopo chechefu, Benki Kuu imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera na maboresho ya kiusimamizi kwa: kusisitiza usimamizi unaozingatia udhibiti wa vihatarishi mbalimbali na kuzitaka benki kuboresha mchakato unaotumika katika kuidhinisha mikopo; kufuatilia taasisi za kibenki ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza mikakati waliyojiwekea katika kupunguza mikopo chechefu; na kuzitaka benki kuwasilisha taarifa za mikopo katika kanzidata ya taarifa za wakopaji.

e) Mwenendo wa Soko la Hisa

17. Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Juni 2024 uliongezeka kwa asilimia 12.1 na kufikia shilingi bilioni 16,834.28 ikilinganishwa na shilingi bilioni 15,010.36 katika kipindi kilichoishia Juni 2023. Kuongezeka kwa mtaji wa Soko la Hisa kumechagizwa na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa. Aidha**,** mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 153.4 na kufikia shilingi bilioni 272.69 ikilinganishwa na shilingi bilioni 107.61 katika kipindi kilichoishia Juni 2023. Kuongezeka kwa mauzo ya hisa kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali.

f) Huduma za Bima

18. Katika mwaka 2023, mali za soko la bima (assets) ziliongezeka kwa asilimia 25.9 kufikia shilingi bilioni 2,144.00 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,679.00 kwa mwaka 2022. Wanufaika wa huduma za bima wameongezeka kutoka wanufaika milioni 17.8 mwaka 2022 hadi wanufaika milioni 23.5 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 32.0. Ongezeko hilo linatokana na Serikali kuendelea kutoa elimu ya masuala ya bima kwa jamii.

1.2.10 Sekta ya Nje

19. Sekta ya nje iliimarika ikichagizwa na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia. Nakisi ya urari wa malipo ya nje ilipungua kwa asilimia 50.2 na kufikia dola za Marekani milioni 2,469.5 mwaka 2023/24 kutoka dola za Marekani milioni 4,955.6 mwaka 2022/23. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 14.7 na kufikia dola za Marekani milioni 14,663.9, ikichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia pamoja na mapato ya utalii. Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 5.6 na kufikia dola za Marekani milioni 16,027.0.

1.3 Deni la Serikali

20. Hadi Juni 2024, deni la Serikali liliongezeka na kufikia shilingi bilioni 96,884.18 ikilinganishwa na shilingi bilioni 81,980.26 Juni 2023. Kati ya deni hilo, deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 64,932.94 na deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 31,951.24. Kuongezeka kwa deni kumetokana na kuendelea kupokelewa

kwa mikopo ya zamani na mipya kwa ajili ya ugharamiaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kupungua kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni.

21. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Juni 2024 na Serikali ikishirikiana na IMF na Benki ya Dunia, imeonesha kuwa deni ni himilivu na viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu. Vilevile, katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa, uwiano wa thamani wa sasa wa deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 35 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55.

1.3.1 Tathmini ya Uwezo wa Nchi Kukopesheka

22. Kwa mwaka 2023/24, kampuni za Fitch Ratings na Moody's Investors Service zilifanya mapitio ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa. Matokeo ya mapitio hayo ni ya kuridhisha, ambapo Moody's imeipandisha nchi daraja kutoka B2 (Positive Outlook) kwenda B1 (Stable Outlook) na Fitch Ratings Services imeendelea na daraja la B *Positive* kama iliyotolewa awali. Matokeo mazuri ya tathmini hizo yanatokana na ukuaji mzuri wa uchumi unaoweza kuhimili mtikisiko wa uchumi, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha mazingira ya biashara na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma.

Kiambatisho Na. 1B

MPANGO KAZI WA KUKABILIANA NA VIHATARISHI

Na	Hatua ya kukabiliana na kihatarishi	Mhusika	Mtekelezaji/watekelezaji	Kiashiria cha upimaji
1.	Kuendelea kutekeleza na kusimamia sera ya fedha na bajeti kwa lengo la kuhakikisha malengo na shabaha za kiuchumi yanafikiwa.	Wizara aya Fedha	Wizara/ Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	Ukuaji na uhimilivu wa viashiria vya uchumi jumla
2.	Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa fedha za Kigeni.	Wizara ya Fedha/Benki Kuu	Wizara/ Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	i. Upatikanaji wa fedha za kigeni ii. Viwango vya kubadilisha fedha
3.	Kuendelea kuhimiza matumizi ya nishati mbadala kama vile nishati ya gesi ili kupunguza athari za kupanda kwa bei ya bidhaa za petroli katika soko la dunia.	Wizara ya Nishati	Wizara/ Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	Kiwango cha usambazaji wa nishati mbadala
4.	Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Kutumia Vyanzo Mbadala ikiwemo kuhusisha sekta binafsi.	Wizara ya Fedha	Wizara/ Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	Idadi ya Miradi iliyotekelezwa kwa kutumia vyanzo mbadala
5.	Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 kwa kutoa dhamana kwenye miradi yenye tija na kufuatilia utendaji wa mashirika kwa mujibu wa	Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Uwekezaji	Wizara/ Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	Malipo ya madeni ya mashirika ya umma yaliyodhaminiwa na serikali

Na	Hatua ya kukabiliana na kihatarishi	Mhusika	Mtekelezaji/watekelezaji	Kiashiria cha upimaji
	mkataba/vigezo/makubaliano ya dhamana husika			
6.	Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa 2022 - 2027 na kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Maafa ili kukabiliana na athari za majanga pindi yanapotokea.	Ofisi ya Waziri Mkuu	Wizara/ Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	i. Bajeti ya Mfuko wa Maafa iii. Bajeti ya Mfuko wa Dharula
7.	Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032).	Ofisi ya Makamu Wa Rais - Muungano na Mazingira	Wizara/ Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	i. Bajeti iliyotengwa kwa uhifadhi na usimamizi wa mazingira ii. Fedha iliyotolewa kwa uhifadhi na usimamizi wa mazingira iii. Hatua zilizochukuliwa za uhifadhi na usimamizi wa mazingira
8.	Kuendelea kutenga rasilimali kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira ili kuhakikisha kilimo kinafanyika kwa vipindi vyote vya mwaka. Aidha, kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa, mbegu bora zinazohimili mabadiliko ya tabianchi, na teknolojia za kuhifadhi chakula ili kupunguza	Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano na Mazingira; Wizara ya Maji; Wizara ya Kilimo,	Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	i. Bajeti iliyotengwa kwa miradi ya umwagiliaji, uhifadhi wa vyanzo vya maji, mazingira na kilimo; na ii. Fedha iliyotolewa kwa miradi ya umwagiliaji, uhifadhi wa vyanzo vya maji, mazingira na kilimo

Na	Hatua ya kukabiliana na kihatarishi	Mhusika	Mtekelezaji/watekelezaji	Kiashiria cha upimaji
	mfumuko wa bei ya chakula.			
9.	Kuendelea kuimarisha usalama katika mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha za umma na shughuli za serikali.	Wizara ya Fedha, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na eGA	Wizara/ Idara Zinazojitegeema, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	i. Hatua zilizochukuliwa za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ii. Ufikiwaji wa lengo la ukusanyaji wa mapato.
10.	Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma za mwaka 2023 ili kudhibiti vitendo vya udanganyifu kwa watumishi wa umma.	Ofisi ya Rais-Mnejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	Wizara/ Idara Zinazojitegeema, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	i. Hatua zilizochukuliwa dhidi ya vitendo vya udanganyifu ii. Kupungua kwa matukio ya udanganyifu kwa watumishi wa umma
11.	Kuendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tahadhari katika taasisi zote za umma ili kubaini changamoto zinazoweza kujitokeza na kuwezesha maamuzi ya kiutendaji kufanyika kwa wakati.	Ofisi ya Waziri Mkuu	Wizara/ Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	i. Watendaji wa vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ii. Mifumo ya ufuatiliaji na tathmini

Kiambatisho Na. 1C

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

2.1 Utangulizi

23. Kiambatisho hiki ni muhtasari wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24. Mapitio yamefanyika katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali kwa kuzingatia malengo na shabaha za bajeti. Maelezo ya kina ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo yanapatikana katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/26.

2.2 Mapato na Matumizi

24. Katika mwaka 2023/24, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi bilioni 44,338.07. Katika kipindi hicho, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 42,920.62 sawa na asilimia 96.7 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 29,829.89 mapato ya ndani sawa na asilimia 95.1 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 31,381.01; shilingi bilioni 5,581.61 ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 102.1 ya lengo la shilingi bilioni 5,466.21; na shilingi bilioni 7,509.11 ni mikopo ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi sawa na asilimia 99.6 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 7,540.84.

25. Katika kipindi hicho, Serikali ilitumia shilingi bilioni 42,945.21 kugharamia utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya Serikali ikiwemo miradi ya kimkakati na kielelezo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 28,308.79 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 14,636.42 ni matumizi ya maendeleo. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 24.59 kiligharamiwa kwa mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ambao upo ndani wigo unaokubalika kisheria. **Jedwali Na. 1** linaonesha mchanganuo wa makadirio ya mapato na matumizi pamoja na ufanisi katika eneo la mapato na matumizi.

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2023/24 (Shilingi bilioni)

	BAJETI	HALISI	UFANISI
Mapato ya ndani	31,381.01	29,829.89	95.1%
TRA	26,725.41	26,072.40	97.6%
Mapato yasiyo ya kodi (MDAs)	3,511.72	2,610.94	74.3%
Mapato ya Halmashauri	1,143.88	1,146.55	100.2%
Misaada	1,111.32	634.69	57.1%
Mikopo nafuu	4,354.89	4,946.92	113.6%
Mikopo ya kibiashara nje	2,100.46	2,101.24	100.0%
Mikopo ya kibiashara ndani	5,440.38	5,407.87	99.4%
Kulipa mtaji	3,542.06	3,662.92	103.4%
kugharamia bajeti (NDF)	1,898.32	1,744.95	91.9%
JUMLA YA MAPATO	**44,388.07**	**42,920.62**	**96.7%**
JUMLA YA MATUMIZI	**44,388.07**	**42,945.21**	**96.7%**
Matumizi ya kawaida	30,310.85	28,308.79	93.4%
Mishahara	10,882.13	9,978.93	91.7%
Kugharamia deni la Serikali	10,469.76	10,752.43	102.7%
Matumizi mengineyo	8,958.96	7,577.43	84.6%
Matumizi ya maendeleo	14,077.22	14,636.42	104.0%
Ndani	10,795.14	11,182.32	103.6%
Nje	3,282.08	3,454.10	105.2%

Chanzo: Wizara ya Fedha

2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/24

26. Utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 umekuwa na mafanikio makubwa katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo:

a) Sekta ya Uchukuzi

27. Katika mwaka 2023/24, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2,157.37 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo jumla ya shilingi bilioni 2,157.37 zilitolewa ikiwa ni sawa na asilimia 100.0 ya bajeti iliyoidhinishwa. Baadhi ya miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa katika mwaka 2023/24 ni:

i. **Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR)**: Shilingi bilioni 1,579.82 zilitolewa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli ya SGR ambapo utekelezaji wake kwa vipande mbalimbali katika Awamu ya Kwanza umefikia hatua zifuatazo: Dar es Salaam – Morogoro (km 300) asilimia 99.1; Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 96.9; Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 59.3; Makutupora – Tabora (km 371) asilimia

14.4; na Tabora – Isaka (km 165) asilimia 5.9. Aidha, hadi Juni 2024, jumla ya vichwa vya treni vya nishati ya umeme 17 na mabehewa 59 ya abiria yamenunuliwa na kuwasili nchini. Vilevile, tarehe 14 Juni, 2024 safari za treni ya abiria katika kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro zilianza.

Serikali iliendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa Awamu ya Pili kwa hatua za awali ambapo utekelezaji uko katika hatua mbalimbali, mathalan Tabora – Kigoma (Km 506) umefikia asilimia 5.84 na mikakati inaendelea kuchukuliwa ili kuanza ujenzi wa vipande vingine.

ii. **Uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania - ATCL**: Katika mwaka 2023/24, shilingi bilioni 270.61 zilitumika katika uboreshaji wa ATCL ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilisha ununuzi wa ndege mbili (2) aina ya Boeing 737 – 9 ambapo moja iliwasili Oktoba 2023 na nyingine Machi 2024; kuendelea na ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA); na kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi za ATCL lililopo katika eneo la kiwanja cha ndege JNIA; kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi za ATCL Makao Makuu Dar es Salaam; na ukarabati wa nyumba 38 za ATCL zilizoko Kiwanja cha Ndege cha KIA.

iii. **Kuendelea na miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu**: Shilingi bilioni 33.96 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika kwa ukarabati wa Meli ya MV Umoja na ujenzi wa Meli ya MV Mwanza "*Hapa Kazi Tu*" umefikia asilimia 96 katika Ziwa Victoria. Aidha, ukarabati wa Meli ya MT. Sangara umefikia asilimia 96 katika Ziwa Tanganyika.

iv. **Miradi ya uboreshaji wa bandari:** Serikali kupitia TPA imeendelea kuboresha bandari zilizozopo katika Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu. Katika Bandari ya Dar es Salaam, kazi zilizofanyika ni pamoja na: uchimbaji wa kina hadi kufikia mita 15.5 na upanuzi wa lango la kuingia na kugeuzia meli hadi kufikia upana wa mita 200, na hivyo kuiwezesha bandari hiyo kupokea meli kubwa zenye urefu wa mita 305. Aidha, uboreshaji wa Bandari ya Tanga katika awamu ya pili umekamilika kwa asilimia 100, ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuboresha magati mawili (2) yenye jumla ya urefu wa mita 450; uboreshaji wa eneo la kuhifadhia makasha lenye ukubwa wa mita za mraba 6,400 na uwezo wa kuhudumia makasha 1,020 TEUs; na ununuzi wa jumla ya mitambo 16 kwa ajili ya kuhudumia shehena.

Serikali pia kupitia TPA imeanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao ambayo ni maalum kwa ajili ya kuhudumia

shehena ya mzigo mchafu (dirty cargo) ikiwemo makaa ya mawe na saruji. Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika mwezi Februari, 2024 na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi zinaendelea. Kuhusu Bandari ya Bagamoyo, Serikali imekamilisha zoezi la kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi lenye ukubwa wa hekta 887. Aidha, uboreshaji wa bandari zilizopo katika Maziwa Makuu umeendelea kwa Bandari ya Kemondo Bay (asilimia 50) na Bandari ya Bukoba (asilimia 65) katika Ziwa Victoria.

v. **Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege:** Serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege nchini kupitia miradi mbalimbali ikiwemo: ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya: Msalato Package I - Miundombinu (asilimia 72.59) - na Package II - Majengo (asilimia 39.42); Musoma (asilimia 57); Iringa (asilimia 99); Kigoma - Awamu ya III (asilimia 10.96); Sumbawanga (asilimia 23); Shinyanga (asilimia 63.15); na Tabora - Awamu III (asilimia 63.8). Serikali ilitoa shilingi bilioni 40.55 kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato na shilingi bilioni 12.7 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vingine vya ndege.

   Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi umefikia asilimia 55; usanifu wa awali wa uboreshaji na upanuzi wa Jengo la Pili la Abiria – JNIA umefikia asilimia 98; na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha ambapo ujenzi wa jengo jipya la abiria pamoja na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA ulifikia asilimia 98. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa majengo mapya ya abiria katika viwanja vya ndege vya Kahama na Kilwa Masoko na ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mpanda ambao umefikia asilimia 97. Pia, ujenzi wa uzio, ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuingia kiwanjani (Access Road) na njia ya watembea kwa miguu (Pedestrian Walkway) kwa kiwango cha lami pamoja na ufungaji wa mfumo na mitambo mipya ya umeme katika Kiwanja cha Ndege Dodoma vimekamilika.

vi. **Uboreshaji wa Vyuo vya Sekta ya Uchukuzi:** Serikali iliendelea kuboresha utoaji huduma za Sekta ya Uchukuzi kwa: kuimarisha miundombinu na kununua vifaa katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kwa kununua Ndege mbili (2) za mafunzo ya urubani; kuendelea na ujenzi wa majengo matano (5) katika Kampasi ya Mabibo – Dar es Salaam yenye madarasa 10, maabara 15, karakana tano (5), mabweni ya wanafunzi mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,504 na ofisi za watumishi 25, ambapo ujenzi wake kwa ujumla umefikia asilimia 75. Aidha, kwa upande wa Chuo cha Bahari (DMI), Serikali ilinunua

mtambo maalum wa kufundishia kwa vitendo (full mission crane simulator) ambao umeanza kutumika kutoa mafunzo kwa vitendo.

b) Sekta ya Nishati

28. Katika mwaka 2023/24, sekta ya nishati iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2,609.15 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambapo shilingi bilioni 2,164.13 zilitolewa, sawa na asilimia 82.9. Miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa ni pamoja na:

i. **Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere - JNHPP (MW 2,115):** ujenzi umefikia asilimia 98.64 ambapo Megawati 705 za umeme zinazalishwa kupitia mitambo mitatu (3) kati ya tisa (9) ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1,244.99 kilitolewa.

ii. **Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400:** kukamilika kwa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rufiji – Chalinze na Kituo cha Kupoza Umeme Chalinze; na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Singida – Arusha – Namanga umefikia asilimia 99.9 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 38.27 kilitolewa.

iii. **Usambazaji wa Umeme Vijijini**: Serikali kupitia REA imeunganisha umeme katika vijiji 12,167 kati ya 12,318 sawa na asilimia 98.8 na vitongoji 32,827 kati ya 64,359 sawa na asilimia 51 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 299.25 kilitolewa.

iv. **Matumizi ya nishati safi ya kupikia:** Kuendelea kuongeza wigo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini kwa kuzindua na kuanza kutekelezwa kwa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 – 2034. Mkakati huo ulizinduliwa rasmi na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 08 Mei, 2024. Aidha, zaidi ya mitungi 100,000 ya gesi ya kupikia (LPG) iligawiwa kwa wananchi katika mwaka 2023/24.

v. **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)**: hatua iliyofikiwa ni ulipaji wa fidia kwa wananchi (asilimia 99.2) na kukamilisha ununuzi wa hisa za Serikali ambapo shilingi bilioni 310.03 zilitolewa. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa makambi na vituo vya kuhifadhia mabomba; ujenzi wa kiwanda cha kuweka mfumo wa joto kwenye mabomba (Thermal Insulation System (TIS) Plant) umefikia asilimia 83; ujenzi wa gati ya kupakilia mafuta eneo la Chongoleani-Tanga umefikia asilimia 47; na mabomba ya kuwezesha kujenga kilomita 700 yameshawasili nchini tayari kwa kuwekewa mfumo wa kuhifadhi joto kabla ujenzi haujaanza. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia wastani wa asilimia 43.5.

c) Sekta ya Ujenzi

29. Utekelezaji wa miradi katika sekta ya ujenzi uliidhinishiwa shilingi bilioni 2,346.09 ambapo shilingi bilioni 2,346.09 zilitolewa sawa na asilimia 100.0. Baadhi ya miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa katika sekta hii ni pamoja na:

i. **Ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja kupitia TANROADS:** Jumla ya km 1,261.06 za barabara kuu na barabara za Mikoa zimejengwa. Kati ya hizo km 417.06 ni barabara za lami na km 844 ni barabara za changarawe. Serikali pia imekamilisha ujenzi wa barabara za juu (flyovers) kwenye makutano ya barabara katika maeneo ya Uhasibu na Chang'ombe Dar es Salaam. Kwa upande wa madaraja, Serikali imeendelea na ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi ambao umefikia asilimia 91 na madaraja mengine matatu (3) ya Sukuma (Mwanza) asilimia 20, Mbangala (Mtwara) asilimia 66 na Mbambe (Pwani) asilimia 25. Aidha, Serikali ilitoa shilingi bilioni 76.96 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi na shilingi bilioni 6.02 kwa ajili ya ujenzi wa madaraja mengine.

ii. **Ujenzi na ukarabati wa barabara za Vijijini na Mijini kupitia TARURA:** Katika mwaka 2023/24, shilingi bilioni 633.48 zilitolewa katika miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara za mijini na vijijini. Jumla ya km 4,202.36 za barabara zimejengwa ambapo kati ya hizo, barabara za lami km 284.40 na barabara za changarawe kilometa 3,917.96. Aidha, ujenzi na ukarabati wa madaraja 75, makalavati 380 na mifereji ya kuondoa maji ya mvua barabarani yenye urefu wa mita 102,351.62 umefanyika. Vilevile, maabara 11 za kupima ubora wa sampuli kama vile udongo, lami na kokoto zinazotumika kujenga miundombinu ili kudhibiti ubora wa kazi za ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara zimeanzishwa katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Tanga, Arusha, Mwanza, Simiyu, Geita, Kigoma, Mtwara, Mbeya na Ruvuma.

vi. **Ujenzi na ukarabati wa vivuko**: vivuko sita (6) vilivyopo katika hatua ya ujenzi ni; Kisorya-Rugezi (asilimia 81), Bwiro-Bukondo (asilimia 87), Mafia-Nyamisati (asilimia 22), Ijinga-Kahangala (asilimia 85), Nyakariro-Kome (asilimia 60) na Buyagu – Mbalika (asilimia 50); na ukarabati wa vivuko vitano (5) vya Mv Magogoni (asilimia 55), Mv Nyerere (asilimia 81), Mv Kilombero II (asilimia 90), Mv Ruhuhu (asilimia 85) na Mv Old Ruvuvu (asilimia 80). Shilingi bilioni 5.34 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vivuko.

vii. **Ujenzi wa barabara kwa ajili ya kupunguza msongamano**; Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam: City Center – Mbagala (km 20.3) umekamilika; City Center – Gongo la Mboto (km 23.3) asilimia 62; Maktaba ya Taifa - Mwenge/Ubungo (km

13.5) asilimia nane (8) na Mwenge - Tegeta (km 15.63) asilimia 10. Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma (km 112.3) ambapo Lot 1 Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Bandari Kavu (km 52.3) asilimia 80.6 na Lot 2 Ihumwa Bandari Kavu – Matumbulu – Nala (km 60) asilimia 76.33; na upanuzi wa barabara ya Uyole – Ifisi - Songwe Airport Jijini Mbeya (km 36) umefikia asilimia 16.3. Aidha, shilingi bilioni 118.21 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Mabasi Yaendayo Haraka, shilingi bilioni 26.39 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mzunguko katika jiji la Dodoma na shilingi bilioni 2.68 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Uyole – Ifisi – Songwe Airport.

d) Sekta ya Kilimo

30. Katika mwaka 2023/24, utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Kilimo uliidhinishiwa shilingi bilioni 829.36 ambapo shilingi bilioni 525.25 zilitolewa sawa na asilimia 63.3. Shughuli za vipaumbele zilizotekelezwa kwa upande wa Sekta ya Kilimo ni pamoja na:

i. **Uzalishaji wa mazao ya kilimo:** Kiasi cha Shilingi bilioni 95.18 zilitolewa na kuwezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa asilimia 11.8 kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2023/24 ambapo tani 22,803,316 zilizalishwa ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 20,402,014 kwa mwaka 2022/23. Aidha, mahitaji ya chakula kwa mwaka 2024/25 ni tani 17,753,989 hivyo, nchi imezalisha ziada ya tani 5,049,327, sawa na utoshelevu wa asilimia 128. Mafanikio haya yametokana na kuongezeka kwa matumizi ya mbolea ya ruzuku kwa wakulima kutoka tani 580,628 mwaka 2022/23 hadi tani 622,054 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 7.13, kuboresha huduma za ugani kwa wakulima kwa kununua vitendea kazi zikiwemo pikipiki 6,444, pamoja na uwepo wa mvua za kutosha katika maeneo mengi nchini. Vilevile, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ulifikia tani 1,263,294 ikilinganishwa na tani 1,109,802 mwaka 2022/23.

ii. **Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora - BBT:** Katika mwaka 2023/24, shilingi bilioni 6.79 zilitolewa na kuwezesha kupatikana kwa mikopo ya riba nafuu yenye thamani ya shilingi milioni 950 kwa vijana 118; kupatikana kwa ekari 340,465.28 katika mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mbeya, Singida, Pwani, Tanga, Njombe na Kagera; kuendelezwa kwa mashamba ya Chinangali II (ekari 1,772) na Ndogowe (ekari 11,430) katika Wilaya ya Chamwino na Mapogoro – Chunya (ekari 52,000); kuajiriwa kwa wahitimu 230 kutoka vyuo vya kilimo kwa ajili ya kutoa huduma za ugani katika maeneo yanayozalisha pamba; na kuchimbwa kwa visima 22 kwa ajili ya umwagiliaji katika mikoa ya Dodoma na Mbeya.

iii. **Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji:** Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji 69 zenye jumla ya hekta 95,005 na mabwawa 14 yenye mita za ujazo 131,535,000 iliyoanza kutekekelezwa mwaka 2022/23 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 50; na kuanza ujenzi na ukarabati wa miradi mipya ya skimu za umwagiliaji yenye jumla ya hekta 143,482 na mabwawa yenye jumla ya mita za ujazo 936,535,700. Katika mwaka 2023/24, shilingi bilioni 144.15 zilitolewa.

iv. **Mradi wa Kudhibiti sumukuvu:** Katika mwaka 2023/24, shilingi bilioni 23.69 zilitolewa katika kudhibiti sumukuvu kwenye mazao ya chakula ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na: ujenzi wa Kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao Baada ya Kuvuna (Mtanana – Kongwa) umefikia wastani wa asilimia 96; ujenzi wa Maabara Kuu ya Kilimo umefikia asilimia 80; kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Kibaiolojia (National Biological Control Unit) kilichopo Kibaha kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa wadudu rafiki na usajili wa viuatilifu hai; kukamilika kwa ghala 14 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 21,500 za mazao; kutolewa kwa mafunzo ya udhibiti wa sumukuvu kwa wakulima 59,485 sawa na asilimia 99.1 ya lengo la kuwafikia wakulima 60,000 na wafanyabiashara 5,547 katika Wilaya 18 nchini; na kutungwa na kupitishwa kwa sheria ndogo za kudhibiti sumukuvu katika Wilaya zote 18 za mradi.

e) Mifugo

31. Utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Mifugo uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 61.92 ambapo shilingi bilioni 15.03 zilitolewa sawa na asilimia 24.3 ya bajeti ya maendeleo. Miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa katika sekta hii ni pamoja na:

i. **Kuimarisha afya ya mifugo:** Katika kudhibiti magonjwa ya mifugo nchini, jumla ya dozi 616,070,986 zilitumika kuchanja mifugo dhidi ya magonjwa 13 ya kipaumbele ambapo jumla ya mifugo 24,114,334 ilichanjwa. Aidha, ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, mbung'o na wadudu wengine, Serikali imeendelea na ujenzi wa majosho 246 ya uogeshaji mifugo katika halmashauri 65 ambapo jumla ya michovyo 1,342,932,142 ya mifugo imefanyika ikiwemo michovyo ya ng'ombe 660,725,421, mbuzi 453,142,239, kondoo 201,975,117 na punda 27,089,365. Jumla ya shilingi bilioni 7.58 zilitolewa.

ii. **Ujenzi wa maabara ya chanjo za mifugo:** Serikali imeendelea na ujenzi wa maabara ya chanjo za magonjwa ya mifugo Kibaha kwa ajili ya uzalishaji wa aina 13 za chanjo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele

ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 25. Jumla ya shilingi milioni 400 zilitolewa.

f) Uvuvi

32. Sekta ya Uvuvi iliidhinishiwa shilingi bilioni 134.41 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 90.42 sawa na asilimia 67.27 zilitolewa. Shughuli na miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa kwa upande wa Sekta ya Uvuvi ni pamoja na**:**

i. **Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko na ununuzi wa meli za uvuvi:** Jumla ya shilingi bilioni 77.79 zilitolewa katika mwaka 2023/24 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha uchimbaji wa kuongeza kina cha maji baharini; utengenezaji wa slab 308; ujenzi wa beam 272; ujenzi wa majengo ya utawala, soko pamoja na sehemu ya kuzalishia barafu, kituo cha kupokea umeme, kituo cha zimamoto na kituo cha kuzalishia maji safi umefikia asilimia 50; ujenzi wa jengo la kuzalishia nitrogen na gati umefikia asilimia 70; na ujenzi wa uzio pamoja na barabara za ndani ya bandari umefikia asilimia 7. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 71. Aidha, katika mradi wa ununuzi wa meli hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa uendeshaji wa meli za uvuvi.

ii. **Ujenzi wa Mialo na Vituo vya Ukuzaji Viumbe Maji:** Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa mialo minne (4) ya Chifunfu (Sengerema), Igombe (Ilemela), Kayenze (Ilemela), Igabilo (Bukoba) ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 46 na Mwalo wa Chato beach asilimia 90. Pia, Serikali imeendelea na ujenzi wa vituo vya ukuzaji viumbe maji vya Ruhila – Songea ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 34, Nyengedi – Lindi asilimia 15, na Rubambagwe – Geita asilimia 63. Ujenzi wa awamu ya kwanza ya kituo cha Ruvula Mtwara umekamilika kwa asilimia 100.

iii. **Ujenzi wa Masoko ya Samaki na Mashamba darasa ya Ukuzaji Viumbe Maji:** Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa masoko mawili (2) ya samaki ya Kasanga – Kalambo ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 90 na soko la Zingibari – Mkinga asilimia 20. Vilevile, kuendelea na ujenzi wa mashamba darasa sita (6) ya ufugaji samaki katika Halmashauri za Njombe asilimia 70, Iringa asilimia 85, Songea asilimia 100, Ruangwa asilimia 60, Kongwa asilimia 80 na Tandahimba asilimia 80. Mashamba darasa manne (4) ya Rombo, Same, Moshi na Mkuranga yapo katika hatua za awali za utekelezaji. Jumla ya shilingi bilioni 2.88 zilitolewa.

g) Sekta ya Madini

33. Katika mwaka 2023/24, Sekta ya Madini iliidhinishiwa shilingi bilioni 90.88 ambapo shilingi bilioni 90.88 zilitolewa sawa na asilimia 100. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na rasilimali madini; kuendelea kwa ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya Tume ya Madini jijini Dodoma ambao umefikia asilimia 90; ununuzi wa vitendea kazi mbalimbali yakiwemo magari na vifaa vya maabara kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi na ukusanyaji maduhuli yatokanayo na rasilimali madini; kuendesha majadiliano ya mikataba ya uendelezaji wa migodi ya uchimbaji madini baina ya Serikali na wawekezaji; maandalizi ya ujenzi wa jengo la Kituo cha *Tanzania Gemmological Centre* (TGC) jijini Arusha; kuwajengea uwezo watumishi wa kituo hicho kwa ajili ya kuimarisha uendeshaji wa mafunzo ya uongezaji thamani madini nchini; na utoaji wa leseni 11,509 za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, uyeyushaji na biashara ya madini na utoaji wa leseni moja (1) ya uchimbaji mkubwa wa madini.

h) Sekta ya Maji

34. Katika mwaka 2023/24, Serikali iliendelea kutekeleza miradi kwenye Sekta ya Maji kwa bajeti iliyoidhinishwa ya jumla ya shilingi bilioni 695.8 ambapo shilingi bilioni 593.4 sawa na asilimia 85.3 zilitolewa. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na: ukamilishaji wa miradi 705 katika vijiji 1,733 na kuwezesha wananchi 4,945,840 kunufaika na huduma na ukamilishaji wa miradi 85 ya maji mijini yenye kunufaisha wananchi 4,641,500. Ukamilishaji wa miradi hiyo umewezesha wastani wa wananchi wanaopata huduma za maji kufikia asilimia 79.6 vijijini na asilimia 90 kwa mijini.

35. Utekelezaji wa miradi ya kimkakati unaendelea ambapo ujenzi wa bwawa la Kidunda umefikia asilimia 27. Vilevile, utekelezaji wa miradi katika miji 28 - kipande cha miji ya Kilwa Masoko na Nanyumbu (asilimia 54); kipande cha miji ya Handeni, Korogwe, Muheza na Pangani (asilimia 49); kipande cha miji ya Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo na Kaliua (asilimia 43); kipande cha Makonde Plateau kwenye miji ya Newala, Nanyamba, Tandahimba na Wilaya ya Mtwara (asilimia 24); kipande cha miji ya Kayanga, Chato na Geita (asilimia 22); kipande cha miji ya Ifakara, Rujewa, Chunya, Njombe, Makambako na Wanging’ombe (asilimia 17); kipande cha mji wa Mafinga (asilimia 16.5); kipande cha miji ya Rorya na Tarime (asilimia 13); kipande cha miji ya Kiomboi, Singida, Manyoni, Mugumu, Chemba na Chamwino (asilimia 9.6); na kipande cha mji wa Songea (asilimia 4.4).

36. Kwa upande wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, shughuli zilizofanyika ni kukarabati vituo 51 na kujenga vituo 11 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji nchini; kukamilisha ujenzi wa mabwawa 14 ya ukubwa wa kati; kujengwa kwa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua katika taasisi 2,413; na kuundwa kwa jumuiya saba (7) za watumia maji. Aidha, jumla ya vyanzo

1,625 vya maji vilihakikiwa ubora wake ambapo matokeo yalionesha kukidhi ubora unaohitajika kwa matumizi ya kiuchumi na kijamii yaliyokusudiwa.

i) Sekta ya Elimu

37. Kwa mwaka 2023/24, Sekta ya Elimu iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 3,449.41 kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi ambapo shilingi bilioni 2,739.83 zilitolewa sawa na asilimia 79.4. Serikali iliendelea na utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ikiwemo:

i. Kuendelea kutekeleza programu ya elimu ya awali, Elimumsingi na Sekondari bila ada; ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika shule za msingi ikiwemo shule mpya 302, vyumba vya madarasa 3,880, mabweni 63 ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, matundu ya vyoo 22,418 na uzio wa mabweni katika shule 88; ukarabati wa madarasa 627 katika shule kongwe za msingi na ukamilishaji wa mabweni saba (7). Kwa upande wa elimu ya Sekondari, Serikali imejenga shule mpya 25, madarasa 6,648, mabweni 444 na matundu ya vyoo 16,795. Pia, imekarabati shule kongwe za sekondari 32, umaliziaji wa maboma ya madarasa 2,441, shule za bweni tisa (9), maabara 132 na matundu ya vyoo 1,650. Jumla ya shilingi bilioni 1,704.37 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na programu hizo.

ii. Serikali imehuisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (Toleo la 2023) sambamba na kuboresha mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na mafunzo ya ualimu pamoja na kusambaza nakala 9,818,251 za vitabu kwa shule za msingi na sekondari.

iii. Katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, Serikali imekamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya Chuo cha Ufundi Dodoma ambapo kitaweza kudahili wanafunzi 1,500 kwa mwaka wa masomo 2024/25 na ujenzi wa vyuo 29 vya mafunzo ya ufundi stadi (wilaya 25 na mikoa 4) ambavyo vimeanza kutoa mafunzo; kuendelea na ujenzi wa vyuo 65 (wilaya 64 na kimoja cha Mkoa wa Songwe) ambapo ujenzi umefikia wastani wa asilimia 35. Vilevile, Serikali imeanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya stashahada wanaosoma fani za kipaumbele ikiwemo afya, sayansi na ufundi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ambapo wanafunzi 2,299 wamenufaika na mikopo. Jumla ya shilingi bilioni 52.1 zilitolewa kwa ajili ya mikopo ya vyuo vya kati pamoja na miradi ya ujenzi.

iv. Katika mwaka 2023/24, Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 786 kwa wanafunzi wa elimu ya juu 229,652 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 569 kwa wanafunzi 198,105 kwa mwaka 2022/23. Aidha, Serikali imetoa ufadhili kwa wanafunzi 1,220 waliofaulu vizuri kidato cha sita katika michepuo ya sayansi kupitia

SAMIA Scholarship ikilinganishwa na wanafunzi 636 kwa mwaka 2022/23 ambapo shilingi bilioni 6.3 zilitolewa kwa ajili ya ufadhili huo.

v. Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika Kampasi 14 za Vyuo Vikuu katika mikoa mbalimbali ambapo hatua iliyofikiwa ni: Chuo Kikuu Ardhi asilimia 48, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya asilimia 35, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Kampasi ya Rukwa asilimia 45 na Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia - Mara asilimia 15. Jumla ya shilingi bilioni 34.75 zilitolewa katika miradi ya ujenzi wa vyuo vikuu.

j) Sekta ya Afya

38. Sekta ya Afya iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1,016.93 ambapo shilingi bilioni 654.07 zilitolewa, sawa na asilimia 64. Serikali ilitekeleza programu na miradi mbalimbali katika Sekta ya Afya iliyolenga kuboresha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na:

i. **Afya ya msingi:** Serikali imeendelea kuboresha huduma za Afya ya Msingi kwa kujenga na kukamilisha miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya zahanati, vituo vya afya na hospitali. Aidha, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ikungi umekamilika na hospitali 33 zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Vilevile, hospitali kongwe 25 zipo katika hatua mbalimbali za ukarabati; vituo vya afya sita (6) vimekamilika; vituo vya afya 16 vipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji; zahanati 40 zimekamilika na zahanati 310 zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Jumla ya shilingi bilioni 237.78 zilitolewa.

ii. **Ngazi ya rufaa:** Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa – Muhimbili umefikia asilimia 95 kwa awamu ya pili, hospitali za Rufaa za Kanda ya Burigi - Chato awamu ya tatu (asilimia 82), Kanda ya Kusini - Mtwara awamu ya kwanza (asilimia 100), Kanda ya Kati - Benjamin Mkapa (asilimia 28); Kanda ya Kaskazini - KCMC (asilimia 71) pamoja na Hospitali Maalum ya Magonjwa Ambukizi – Kibong’oto awamu ya pili (asilimia 85). Hospitali nne (4) kati ya nane (8) za Rufaa za Mikoa ujenzi wake umekamilika kwa awamu ya kwanza katika mikoa ya Geita, Simiyu, Songwe na Mbeya. Hospitali 4 za Rufaa za Mikoa za Maweni – Kigoma (asilimia 98), Mara (asilimia 95), Manyara (asilimia 86) na Mawenzi – Kilimanjaro (asilimia 86). Jumla ya shilingi bilioni 25.57 zilitolewa.

iii. **Dawa, Vifaa tiba na Chanjo**: Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya kwa kuhakikisha kuwa bidhaa za afya na chanjo muhimu zinapatikana na kuwafikia wananchi kwa wakati. Upatikanaji wa huduma

za dawa muhimu ulifikia wastani wa asilimia 85 na chanjo muhimu ulifikia wastani wa asilimia 91. Jumla ya shilingi bilioni 293.56 zilitolewa.

iv. **Bima ya Afya kwa Wote**: Serikali imetunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura 161 ambayo ilipitishwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba, 2023 ambapo kanuni za sheria hiyo zimeidhinishwa na kutangazwa kupitia Tangazo la Serikali Namba 809 mwaka 2024 kwa ajili ya kuanza kutumika.

k) Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara

39. Katika mwaka 2023/24, shilingi bilioni 132.09 ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli na miradi ambapo shilingi bilioni 121.9 zilitolewa sawa na asilimia 92.3. Shughuli na miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:

i. **Uwekezaji:** Miradi 9,678 ya uwekezaji yenye thamani ya dola za Marekani milioni 8,658 imesajiliwa katika kipindi cha mwaka 2023 ikilinganishwa na miradi 8,401 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 5,658.47 kwa mwaka 2022; kuanzishwa kwa Mfumo wa Kieletroniki wa kuhudumia wawekezaji "**Tanzania Electronic Investment Window" (TeIW)** unaowezesha wawekezaji kusajili miradi wakiwa ndani au nje ya nchi na kupata vibali vya uwekezaji baada ya kukidhi vigezo; kukamilishwa kwa tafiti kuhusu maeneo maalumu ya kiuchumi (SEZ) na mwongozo wa uendelezaji na usimamizi wa maeneo hayo.

ii. **Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (Blueprint):** kufanya marekebisho ya Sheria na Kanuni 55 katika sekta za uwekezaji, viwanda, biashara, kilimo, ufugaji, maliasili na utalii; kuondolewa kwa tozo, ada na faini 67 ambazo zilikuwa kero katika uwekezaji kwenye sekta mbalimbali; na kupungua kwa idadi ya siku za kupata huduma kwa wafanyabiashara na wananchi mathalan mamlaka za Serikali zimepunguza muda wa kutoa leseni na usajili kutoka wastani wa siku 14 hadi 3.

iii. **Viwanda:** Shughuli mbalimbali zimetekelezwa ikiwa ni pamoja na: Kuanzisha kongani ya Kisasa ya Viwanda (Modern Industrial Park) – Pwani; kukamilisha ujenzi wa viwanda viwili (2) katika Kongani ya Viwanda ya Kwala – Pwani ambavyo ni kiwanda cha nguo cha House of Garments kilichoajiri wafanyakazi 50 na kiwanda cha KVS Chemicals ambacho kina jumla ya wafanyakazi 25; Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya msingi katika Kongani ya Viwanda – TAMCO Kibaha; kuwalea na kuwakuza wajasiriamali watano (5) kupitia SIDO ambao kwa sasa ni wamiliki wa viwanda vya Akross Ltd – Mtwara, Kigoma Tansoap Enterprises – Kigoma, Choice Coffee – Kilimanjaro, BAKEL Company

Ltd- Dodoma na Double Natural Products – Mbeya; na kutoa mikopo ya shilingi bilioni 108.43 kwa viwanda 37 kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).

Aidha, Serikali imeendelea na jitihada za kuhamasisha ujenzi na uanzishwaji wa viwanda ambapo jumla ya viwanda 13 vya magari katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam vimeanzishwa. Kadhalika, viwanda vya vioo vitatu (3) vimekamilika na kuanza uzalishaji wa bidhaa za vioo katika mikoa ya Pwani na Dar es salaam. Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 1,625 na zisizo za moja kwa moja 3,857.

iv. **Biashara:** Mikopo 956 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.3 imetolewa kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (National Enterpreneurship Development Fund - NEDF) kwa wanawake ili kusaidia biashara ndogo kwa miradi ya vijijini; kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara ambapo jumla ya kampuni 10,651 zimesajiliwa kati ya 15,000 zilizokusudiwa, sawa na asilimia 71; kusajili majina ya biashara 19,040 kati ya 28,000 yaliyopangwa, sawa na asilimia 68; kusajili alama za biashara na huduma 1,998 kati ya 4,200 zilizokuwa zimepangwa, sawa na asilimia 48; na ukusanyaji wa mazao tani 371,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 905 kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani. Aidha, katika kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi, nyama tani 4,497.7 zenye thamani ya shilingi bilioni 56.6 ziliuzwa katika soko la Saudi Arabia, Qatar na Umoja wa Falme za Kiarabu - U.A.E.

l) Utawala Bora

40. Katika mwaka 2023/24, shughuli na miradi mbalimbali zilitekelezwa ikiwa ni pamoja na:

i. **Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2024:** Serikali imeendelea na maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 kwa kutekeleza yafuatayo; ununuzi wa vifaa vya uchaguzi, kufanya vikao na kupokea maoni ya wadau mbalimbali na uhakiki wa maeneo ya utawala awamu ya kwanza katika Halmashauri 184 ambapo shilingi bilioni 12.25 zilitolewa.

ii. **Uendelezaji wa mji wa Serikali Mtumba**: Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu na majengo ya ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma ambapo jumla ya shilingi bilioni 386.07 zilitolewa. Majengo ya Wizara ya Maji, Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais – MUUUB yamekamilika na yameanza kutoa huduma. Awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi za Wizara 26, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao umefikia wastani wa asilimia 84.1.

iii. **Utoaji wa Haki**: Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki ikijumuisha ujenzi wa miundombinu na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa mashauri ya mahakama. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki katika mikoa sita (6) ambayo ni Katavi, Ruvuma, Songwe, Njombe, Simiyu na Geita; ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama Dodoma umefikia asilimia 97.3; ujenzi wa Mahakama za Wilaya ya Ulanga, Kwimba na Liwale; na ujenzi wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo Usevya (Mlele), Nyakibimbili (Bukoba), Mahenge (Kilolo), Newala Mjini (Newala), Madale (DSM), Kinesi (Rorya) na Luilo (Ludewa). Miradi mingine ni; Kuendelea na ujenzi wa nyumba 48 za Majaji eneo la Iyumbu Dodoma. Aidha, Tanzania imefanikiwa kuwa mwenyeji wa mikutano ya kimataifa ya masuala ya utoaji wa haki ikiwemo kikao cha 77 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu pamoja na Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa nchi za Jumuiya ya Madola.

iv. Ujenzi wa nyumba za viongozi na watumishi: Serikali imeendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili inayohusisha ujenzi wa nyumba 150 za watumishi eneo la Nzuguni jijini Dodoma ambao umefikia asilimia 25; ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma katika eneo la Magomeni Kota Awamu ya Pili “Block B” umefikia asilimia 96; na ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma za Temeke Kota jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 33. Kwa upande wa nyumba za viongozi, Serikali imeendelea na ukarabati wa nyumba tano (5) za viongozi jijini Dodoma na nyumba tano (5) za viongozi katika mikoa mingine. Katika utekelezaji wa miradi hiyo, shilingi bilioni 3.94 zilitolewa.

Serikali kupitia OR - TAMISEMI imeendelea na ujenzi na ukarabati wa nyumba 69 za viongozi ngazi ya mikoa na wilaya ambapo nyumba 14 zimekamilika na nyumba 55 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, Serikali imeendelea na ujenzi wa nyumba 144 kwa ajili ya wakurugenzi na wakuu wa idara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Shilingi bilioni 32.47 zilitolewa.

v. **Kuimarisha na kukuza Demokrasia Nchini**: Katika jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia nchini, Bunge lilitunga Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2024. Aidha, marekebisho yamefanyika katika Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2023 na Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258. Vilevile, Serikali imeendelea na zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

vi. **Ulinzi na Usalama**: Serikali imeendelea kuimarisha na kusimamia hali ya ulinzi na usalama wa mipaka nchini kwa kuvipatia vyombo vya ulinzi na usalama vifaa vya kisasa na mafunzo. Katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao, Serikali imejenga jumla ya vituo 26 vya polisi vya daraja A, B na C; ofisi sita (6) za makamanda wa polisi wa mikoa na ujenzi na ukarabati wa nyumba 57 za mapumziko na makazi.

vii. **Ujenzi wa majengo ya utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa:** Serikali imeendelea na ujenzi wa majengo 75 ya utawala ya Halmashauri ambapo majengo ya utawala 24 ya Halmashauri za Madaba, Sikonge, Ruangwa, Rombo, Babati, Tanganyika, Buhigwe, Mtwara, Newala, Morogoro, Misungwi, Nsimbo, Busokelo, Mlele, Chamwino, Uyui, Bumbuli, Momba, Chunya, Kalambo, Nyasa, Kakonko, Songwe na Manispaa ya Kigamboni yamekamilika na majengo mengine 51 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo shilingi bilioni 49.65 zilitolewa.

viii. **Ujenzi wa Ofisi za Watendaji Kata na Vijiji:** Serikali imeendelea kujenga jumla ya ofisi 295 katika ngazi ya kata, mitaa na vijiji. Ujenzi huo unajumuisha ofisi 137 za watendaji wa kata, 67 za vijiji na 91 ofisi za mitaa. Ujenzi wa ofisi 95 umekamilika ambapo ofisi 24 za watendaji kata, ofisi 19 za watendaji wa vijiji na ofisi 48 za watendaji wa mitaa. Aidha, ofisi 200 zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Jumla ya shilingi bilioni 4.3 zilitolewa.

m) Sekta ya Ardhi

41. Katika mwaka 2023/24, utekelezaji wa shughuli na miradi uliidhinishiwa shilingi bilioni 461.05 ambapo shilingi bilioni 434.50 zilitolewa, sawa na asilimia 94.3. Shughuli na miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa ni pamoja na: kubuni na kusanifu miji ya Satelaiti miwili (2) katika majiji ya Dodoma (Msalato) na Arusha (Afcon City) ili kuwa na miji nadhifu na kudhibiti makazi holela; kusajili Hatimiliki kutoka 76,746 mwaka 2022 hadi 87,240 Juni, 2024; kuimarisha mipaka ya kimataifa kati ya Tanzania na Burundi yenye urefu wa km 100 na kati ya Tanzania na Kenya yenye urefu wa km 80 kwa kujenga na kuongeza alama, kupima, kukarabati, kuandaa ramani na mikataba ya mipaka; kuimarisha usimamizi wa mipaka ya Hifadhi kwa kusimika vigingi 32,838 kuzunguka maeneo ya Hifadhi za Taifa 21, Mapori ya Akiba 29 na Hifadhi za Misitu 416; kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi ya Halmashauri za wilaya tatu (3) za Hanang, Ngorongoro na Msomera-Handeni; na usimikaji wa miundombinu wezeshi ya TEHAMA katika Halmashauri 44 umekamilika na Halmshauri 41 usimikaji unaendelea.

n) Sekta ya Utalii

42. Katika mwaka 2023/24, sekta hii iliidhinishiwa shilingi bilioni 692.67 ambapo hadi Juni 2024, shilingi bilioni 657.37 zilitolewa sawa na asilimia 94.9. Serikali imeendelea kuboresha sekta ya utalii ambapo idadi ya watalii wa nje na ndani waliotembelea vivutio mbalimbali imeongezeka. Idadi ya watalii wa nje ilifikia 1,808,205 mwaka 2023 kutoka 1,454,920 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 24.3 na kupelekea ongezeko la mapato kufikia dola za Marekani bilioni 3.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 2.5 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 33.5. Aidha, idadi ya watalii wa ndani ilifikia 1,976,009 mwaka 2023 kutoka 1,084,737 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 82.2 na kupelekea ongezeko la mapato kufikia shilingi bilioni 175.3 mwaka 2023 kutoka shilingi bilioni 120.3 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 45.7.

43. Mafanikio haya yametokana na; kuimarika kwa utoaji wa huduma, utangazaji wa vivutio vya utalii kupitia programu ya Tanzania The Royal Tour; maonesho ya kimataifa (Road Shows); ziara za mafunzo (fam trips); kuimarika kwa miundombinu ya utalii ikiwemo barabara na viwanja vya ndege pamoja na kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa kupanua wigo wa mazao ya utalii kama vile utalii wa meli na fukwe na kufanikiwa kufikia nchi nyingi na masoko mapya.

o) Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - PPP

44. Katika mwaka 2023/24, Serikali ilianzisha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP Centre) baada ya marekebisho ya Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103. Katika kipindi hicho, Serikali ilipokea na kuchambua miradi mitano (5) ambayo ipo katika hatua ya ununuzi: Mradi wa barabara ya tozo kutoka Kibaha - Chalinze kilometa 78.9; ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na ujenzi wa Kituo cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; mradi wa ukaguzi wa vyombo vya moto kutoka Shirika la Uzalishaji mali la Jeshi la Polisi na mradi wa Uendeshaji wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Kwanza (Kimara - Morocco – Gerezani - Kivukoni). Aidha, miradi 74 ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi ikiwemo upembuzi yakinifu. Vilevile, Serikali iliendelea kutoa mafunzo katika Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na Taasisi za Fedha kuhusu dhana ya PPP, Sheria ya PPP na Kanuni zake kwa wadau 555. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wadau katika uibuaji, uandaaji, ugharamiaji na utekelezaji wa miradi ya PPP.

2.4 Fursa zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti

45. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 fursa zilizojitokeza ni pamoja na:

i. Uwepo wa teknolojia na miundombinu inayowezesha malipo bila kutumia

fedha taslimu *(cashlite economy)* na kurahisisha upatikanaji wa huduma na ukusanyaji wa mapato;

ii. Kuongezeka kwa soko la ndani la bidhaa mbalimbali kutokana na ongezeko la kipato na idadi ya watu;

iii. Ongezeko la watalii wa nje na ndani wanaotembelea vivutio vya utalii;

iv. Ongezeko la mahitaji ya chakula katika soko la dunia;

v. Ongezeko la umeme unaozalishwa na kuingizwa katika Gridi ya Taifa kutokana na kuendelea kukamilishwa kwa ufungwaji wa mitambo ya kuzalisha umeme katika Mradi wa JNHPP (MW 2,115);

vi. Uwepo wa gesi asilia inayozalishwa nchini kwa ajili ya matumizi ya viwandani, majumbani, kwenye magari na taasisi;

vii. Uwepo wa idadi kubwa ya vijana wanaoweza kutumika kama nguvukazi ya Taifa;

viii. Uwepo wa masoko ya mitaji;

ix. Uwepo wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo reli ya kisasa (SGR), viwanja vya ndege na barabara;

x. Ukuaji wa miji ambao umekuwa ukifungua fursa nyingi za kiuchumi;

xi. Ongezeko la bei ya madini na vito vya thamani katika soko la dunia;

xii. Uwepo wa mazingira wezeshi ya kuanzishwa kwa miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa PPP kutokana na mabadiliko ya Sheria ya PPP ya mwaka 2023; na

xiii. Uwepo wa amani, umoja na utulivu.

2.5 Changamoto Zilizojitokeza katika Utekelezaji wa Bajeti

46. Pamoja na mafanikio katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 changamoto zilizojitokeza ni:

i. Kupanda kwa bei ya mafuta na mbolea katika soko la dunia;

ii. Uwepo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kodi kwa kuingiza bidhaa nchini kupitia njia mbalimbali za udanganyifu zikiwemo magendo;

iii. Mwitikio mdogo wa kutoa na kudai stakabadhi za kielektroniki za EFD wakati wa mauzo;

iv. Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu wa ubia na sekta ya umma (PPP);

v. Ushiriki mdogo wa watanzania katika miradi inayotekelezwa (*local content*);

vi. Matumizi makubwa ya nishati isiyo safi (kuni na mkaa) katika kupikia hivyo kuathiri mazingira na afya za watumiaji;

vii. Upungufu wa fedha za kigeni nchini ikichangiwa na mabadiliko ya sera za kifedha katika nchi zilizoendelea;

viii. Kuathirika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma kutokana na migogoro ya kikanda na kimataifa;

ix. Kuongezeka kwa viwango vya riba kwenye masoko ya fedha ya kimataifa; na

x. Mabadiliko ya tabianchi na athari zake zilizosababisha magonjwa ya

mlipuko, mafuriko na maporomoko ya ardhi.

2.6 Hatua za Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti

47. Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto zilizojitokeza. Miongoni mwa hatua hizo ni:

i. Kuendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza bei ya mbolea na gharama za uzalishaji wa mazao;
ii. Kufanya ununuzi wa mafuta kwa kutumia sarafu mbadala ikiwemo Euro, paundi ya Uingereza, shilingi ya Tanzania na Dirham ya UAE;
iii. Kuendelea kuboresha mazingira ya ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ikiwemo kutoa elimu kuhusu dhana ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi;
iv. Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia Mwaka 2024 – 2034;
v. Kuweka mazingira wezeshi yatakayo chochea ushiriki wa wananchi katika miradi inayotekelezwa;
vi. Kupanua wigo wa kodi kwa kufanya maboresho kwenye sheria za kodi yaliyoanzisha utaratibu wa ukusanyaji wa kodi kwa wachimbaji wadogo wa madini, pamoja na kuendelea kuongeza wigo kwenye huduma zitolewazo kwa njia ya mtandao na makampuni yasiyo wakazi nchini;
vii. Kuendelea kuhamasisha matumizi ya mashine za risiti za kielektroniki ikiwemo kampeni ya TUWAJIBIKE;
viii. Kufanya maboresho katika Mfumo wa Usimamizi wa Mapato ya Forodha (TANCIS) wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuongeza ufanikishaji wa biashara za kimataifa;
ix. Kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa;
x. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Kodi za Ndani (IDRAS) ambao ni mahsusi kwa ajili ya kuboresha usajili wa walipakodi, ukusanyaji wa kodi na ufuatiliaji wa walipakodi.
xi. Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuongeza Upatikanaji wa Fedha za Kigeni;
xii. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu kutumia fursa ya uwepo wa masoko ya mitaji;
xiii. Kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa Mwaka 2021;
xiv. Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa 2022 - 2027 na kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Maafa ili kukabiliana na athari za majanga pindi yanapotokea;
xv. Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuimarisha usimamizi na uendelevu wa rasilimali za maji; na
xvi. Kuendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya kisekta kwa ajili ya kutumia kikamilifu fursa zinazotokana na faida ya jiografia ili kufikia masoko ya EAC, SADC na COMESA ikiwemo ujenzi wa reli ya SGR, uboreshaji wa bandari na ujenzi wa bandari kavu, ujenzi na

ukarabati wa barabara zinazounganisha shoroba za nchi na nchi, ununuzi wa ndege za abiria na mizigo na ujenzi wa njia za umeme za msongo mkubwa (kV 400).

2.7 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25

Mapato

48. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, Serikali imekusanya shilingi bilioni 11,553.33 kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 7,930.02 ni mapato ya ndani, sawa na asilimia 99.4 ya lengo la shilingi bilioni 7,976.35. Mapato hayo yanajumuisha mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania shilingi bilioni 7,090.38, mapato yasiyo ya kodi yaliyokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea shilingi bilioni 518.32 na shilingi bilioni 321.32 ni mapato kutoka vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

49. Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa mwaka 2024/25. Mikakati hiyo ni pamoja na; kuendelea kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato na kuhamasisha matumizi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki kupitia uendeshaji wa program mbalimbali za hamasa ikiwemo kuanzisha Tunu ya Uzalendo.

50. Misaada na mikopo nafuu ilifikia shilingi bilioni 1,373.09, sawa na asilimia 118.5 ya lengo la shilingi bilioni 1,159.18. Aidha, mikopo ya kibiashara kutoka masoko ya ndani ilifikia shilingi bilioni 1,656.56, sawa na asilimia 97.8 ya lengo la shilingi bilioni 1,694.35. Mikopo ya kibiashara kutoka nje ilifikia shilingi bilioni 593.65, sawa na asilimia 79.5 ya lengo la shilingi bilioni 746.78. Serikali itaendelea kutekeleza makubaliano yaliyoainishwa kwenye mikataba ili Washirika wa Maendeleo waweze kutoa fedha za misaada na mikopo nafuu kulingana na makubaliano.

Matumizi

51. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25, ridhaa ya shilingi bilioni 11,667.53 ilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 7,549.62 na matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 4,117.91. Ridhaa za matumizi ya kawaida zinajumuisha: mishahara shilingi bilioni 2,735.75; kugharamia deni la Serikali shilingi bilioni 2,366.37; na matumizi mengineyo shilingi bilioni 2,447.50. Fedha za maendeleo zinajumuisha shilingi bilioni 3,199.78 fedha za ndani na shilingi bilioni 918.13 fedha za nje. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 114.20 kiligharamiwa kwa mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ambao upo ndani ya wigo unaokubalika kisheria.

52. Fedha za matumizi ya maendeleo zilitolewa kugharamia miradi na programu mbalimbali ikiwemo: ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) shilingi bilioni 209.29; ujenzi na ukarabati wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege shilingi bilioni 600.66; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - JNHPP (MW 2,115) shilingi bilioni 83.78; miradi ya umwagiliaji shilingi bilioni 72.84; Programu ya Elimumsingi bila ada shilingi bilioni 121.06; Kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania shilingi bilioni 355.04; Mitihani ya darasa la saba pamoja na kidato cha nne shilingi bilioni 131.95 na mradi wa usambazaji umeme vijijini shilingi bilioni 99.48.

53. Serikali imeendelea na maandalizi ya mashindano ya kuwania Kombe la Mataifa ya Afrika yatakayofanyika nchini mwaka 2027 kwa kuanza ujenzi wa kiwanja cha michezo katika Jiji la Arusha ambapo jumla ya shilingi bilioni 50.78 zimetolewa. Vilevile, shilingi bilioni 212 zimetolewa kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024, na shilingi bilioni 123.9 zimetolewa kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Kiambatisho Na. 1D

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

3.1 Utangulizi

54. Sehemu hii inaelezea mapitio ya utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25 kwa kuzingatia tathmini na uchambuzi wa bajeti za mafungu ya kisekta kwa mwaka 2024/25 na maoni ya wadau yaliyotolewa katika vikao mbalimbali kuhusu maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

3.2 Sura ya Bajeti ya Mwaka 2024/25

55. Kufuatia vipaumbele vya Serikali na maboresho mbalimbali ya kisera na mifumo ya ukusanyaji mapato yaliyofanyika, Sura ya bajeti ya Serikali ilibadilika kutoka mapendekezo ya shilingi bilioni 47,424.9 hadi shilingi bilioni 49,345.7 sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Sababu za ongezeko hilo ni kuimarika kwa mwenendo wa makusanyo ya mapato ya ndani pamoja na misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. **Jedwali Na.3.1** linaonesha mapendekezo ya Sura ya Bajeti pamoja na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2024/25.

Jedwali Na.3.1: Mapendekezo ya Sura ya Bajeti pamoja na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2024/25

				Shilingi Bilioni
	Mapato	**2024/25 Mwongozo**	**2024/25 Bajeti Iliyoidhinishwa**	**Ongezeko/ Upungufu**
		A	**B**	**B - A**
A.	**Mapato ya Ndani-Serikali Kuu**	**33,120.70**	**33,254.31**	**133.60**
	(i) Mapato ya Kodi na yasiyo ya kodi (TRA)	*29,520.69*	*29,415.29*	-105.40
	(ii) Mapato yasiyo ya kodi	*3,600.02*	*3,839.02*	239.00
B.	**Mapato ya Halmashauri**	***1,315.47***	***1,356.34***	**40.87**
C.	**Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo**	**4,291.86**	**5,130.61**	**838.75**
	(i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS	*851.02*	*1,489.77*	638.75
	(ii)Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi	*3,313.96*	*3,461.95*	147.99
	(iii)Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta	*126.88*	*178.89*	52.01
D.	**Mikopo ya Ndani na Nje**	**8,696.87**	**9,604.43**	**907.56**
	(i) Mikopo ya Nje	*2,555.00*	*2,986.64*	431.64
	(ii) Mikopo ya Ndani	*2,222.05*	*2,595.42*	373.36
	(iii)Mikopo ya Ndani- Rollover	*3,919.81*	*4,022.37*	102.56
E.		*0.00*	*0.00*	0.00
	JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D+E)	**47,424.90**	**49,345.69**	**1,920.79**
	Matumizi			
F.	**Matumizi ya Kawaida**	**33,333.82**	**33,386.32**	**52.51**
	(i) Mfuko Mkuu wa Serikali	**14,715.97**	**15,736.28**	**1,020.31**
	-Malipo ya Riba Ndani	*3,025.49*	*3,146.67*	*121.18*
	-Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover)	*3,919.81*	*4,022.37*	*102.56*
	-Malipo ya Mtaji Nje	*3,388.53*	*3,517.12*	*128.59*
	- Malipo ya Riba Nje	*1,767.33*	*2,435.31*	*667.98*
	- Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii	*2,000.00*	*2,000.00*	*0.00*
	-Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu	*614.81*	*614.81*	*0.00*
	(ii) Mishahara	***11,774.85***	***11,767.99***	**-6.86**
	(iii) Matumizi Mengineyo (OC)	***5,608.94***	***5,882.06***	**273.12**
	- Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa	*200.00*	*200.00*	*0.00*
	- Matumizi ya Halmashauri (own source)	*793.23*	*815.06*	*21.84*
	- Matumizi mengineyo	4,615.71	4,866.99	251.28
	(iii) Ruzuku ya Maendeleo	1,234.06	0.00	-1,234.06
	-Bodi ya Mikopo	832.42		-832.42
	-Elimumsingi bila Ada	401.64		-401.64
G.	**Matumizi ya Maendeleo**	**14,091.09**	**15,959.36**	**1,868.28**
	(i) Fedha za Ndani	*10,650.25*	*12,318.53*	*1,668.28*
	o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa	*400.00*	*400.00*	*0.00*
	o/w Ugharamiaji wa SGR	*1,800.00*	*1,511.00*	*-289.00*
	o/w Ugharamiaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere	*710.00*	*620.00*	*-90.00*
	o/w Matumizi ya Halmashauri (own Source)	*522.24*	*541.28*	*19.04*
	o/w Miradi mingine	*7,218.01*	*8,057.19*	*839.18*
	o/w Bodi ya Mikopo	*0.00*	787.42	
	o/w Elimumsingi bila Ada	*0.00*	401.64	
	(ii) Fedha za Nje	*3,440.84*	*3,640.84*	*200.00*
	JUMLA YA MATUMIZI YOTE (F+G)	**47,424.90**	**49,345.69**	**1,920.78**
	NAKISI YA BAJETI (asilimia ya Pato la Taifa)	**2.2%**	**2.9%**	

Chanzo: Wizara ya Fedha

3.3 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25

a) Uandaaji wa Mpango na Bajeti

56. Katika uandaaji wa mipango na bajeti, mafungu yameendelea kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2024/25 pamoja na mipango mikakati ya mafungu husika. Mafungu yamezingatia uingizaji takwimu sahihi za GFS kwenye mifumo ya kibajeti na uzingatiaji wa ratiba ya maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25 ikiwemo mawasilisho ya MTEF na

randama kwa wakati. Aidha, Kamati za Bajeti zimeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 17(2).

.

b) Ukusanyaji wa Mapato

57. Maafisa Masuuli wameendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa ikiwa ni pamoja na kutumia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) na kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348. Aidha, Serikali kupitia OR - TAMISEMI imeunda timu ya tathmini ya vyanzo vya mapato kwa kila Halmashauri ili kuziwezesha kuwa na makadirio yenye uhalisia ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kufikia malengo yaliyokusudiwa. Tathmini hiyo imewezesha kuongezeka kwa makadirio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kutoka shilingi bilioni 1,143.88 mwaka 2023/24 hadi shilingi bilioni 1,356.34 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 15.66. Vilevile, imebainika kuwa ipo haja ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha kufanya tathmini ya vyanzo vya mapato kwa mafungu mengine ili kuwa na makadirio ya ukusanyaji wa mapato yenye uhalisia.

c) Kiwango Cha Kubadilishia Fedha

58. Katika maandalizi ya Mpango na Bajeti Mafungu na Taasisi zilizingatia kiwango elekezi cha ubadilishaji fedha za kigeni cha dola moja ya Marekani kwa Shilingi za Tanzania 2,555.00 kilichobainishwa katika Mwongozo. Hata hivyo, kumekuwepo na ongezeko la thamani ya dola ya Marekani katika utekelezaji wa mpango na bajeti.

d) Maandalizi ya Ikama na Bajeti ya Mishahara

59. Maafisa Masuuli wameendelea kuandaa ikama za bajeti ya mishahara kwa mujibu wa Mwongozo wa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

e) Maandalizi ya Makadirio ya Bajeti ya Matumizi Mengineyo

60. Mafungu pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa yametenga fedha katika bajeti ya 2024/25 kwa ajili ya; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kugharamia shughuli za usimamizi wa vihatarishi, kugharamia mabadiliko ya miundo ya Taasisi, kugharamia shughuli za uendeshaji wa ofisi na kulipa stahili za kisheria kwa watumishi na kuwajengea uwezo watumishi.

f) Maandalizi ya Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

61. Mafungu yaliwasilisha Wizara ya Fedha takwimu za fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ambazo zilisaidia katika maandalizi sahihi ya ukomo wa bajeti za mafungu. Wizara za Kisekta zilijumuisha bajeti za shughuli zinazotekelezwa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kinyume na maelekezo ya Mwongozo. Aidha, baadhi ya mafungu yameendelea kutenga bajeti kwenye miradi mipya kabla ya kukamilisha miradi inayoendelea.

g) Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni

62. Utekelezaji wa Sheria ya Benki Kuu, Sura 197, Sheria ya Kubadilisha Fedha za Kigeni, Sura 271 na Kanuni zake na Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni umeimarishwa kwa kudhibiti matumizi holela ya fedha za kigeni, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kupiga marufuku ununuzi unaofanywa kwa kutumia fedha za kigeni nchini. Hata hivyo, imebainika kuwa fedha za kigeni zimeendelea kutumika hususan katika ununuzi wa bidhaa na huduma ndani ya nchi.

h) Uzingatiaji Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

63. Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 katika uandaaji wa mipango na ugawaji wa rasilimali. Aidha, wakati wa mapitio ya utekelezaji imebainika kuwa baadhi ya mafungu hayakutumia takwimu hizo ipasavyo katika kuandaa mipango.

i) Uzingatiaji Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana

64. Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 imeendelea kuzingatiwa. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya baadhi ya mafungu kutumia fedha za misaada na mikopo kwa matumizi tofauti na ilivyokuwa kwenye mpangokazi ulioidhinishwa kulingana na kanuni namba 5 ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 inayotaka mikataba yote ya mikopo na misaada itakayosainiwa kuzingatia miradi ya kimkakati inayozalisha mapato (investment projects) na maeneo ya vipaumbele.

j) Uzingatiaji wa Masuala ya Muungano

65. Maafisa Masuuli wameendelea kushughulikia masuala ya Muungano ikiwemo kutenga bajeti ili kuimarisha Muungano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) sambamba na kuendelea kubadilishana ujuzi katika masuala ya kiuchumi, kimaendeleo na kijamii. Aidha, Muungano umeendelea kuimarika ambapo Serikali zote mbili zimefanikiwa kusimamia utekelezaji wa masuala ya muungano kwa ufanisi na kuleta mafanikio ikiwemo kuimarika kwa utaifa, umoja, amani, utulivu na hali ya maisha ya wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi wa pande zote mbili za Muungano.

k) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

66. Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) wa Mwaka 2017/18-2024/25 na mpangokazi wake ili kuboresha mahusiano yaliyopo baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Aidha, Maafisa Masuuli wameendelea kuwasilisha Hazina makadirio ya michango ya uanachama wa kikanda na kimataifa kwa ajili ya kujumuishwa kwenye bajeti.

l) Uchumi wa Buluu

67. Maafisa Masuuli wameendelea kuibua fursa zitokanazo na rasilimali za maji bahari na baridi na kuweka mipango na mikakati itakayowezesha fursa hizo kutumika kikamilifu kwa lengo la kuongeza mchango katika mapato ya Serikali, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Baadhi ya fursa zilizobainishwa ni wingi na mtawanyiko wa samaki uliopo katika ukanda wa uchumi wa bahari (deep sea fishing), madini yaliyopo kwenye sakafu ya bahari, mafuta na gesi na ujenzi na upanuzi wa bandari. Hata hivyo, imebainika kuwa bado fursa hizo hazijatumika ipasavyo.

m) Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

68. Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004, sheria na miongozo kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuwezesha makundi ya watu wenye mahitaji maalum.

n) Uandaaji wa Bajeti yenye Mlengo wa Kijinsia

69. Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia maelekezo ya kuandaa bajeti yenye mlengo wa kijinsia. Hata hivyo, imebainika baadhi ya mafungu kutotenga na baadhi kutenga bajeti zisizotosheleza kwa ajili ya kutekeleza masuala ya kijinsia.

o) Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

70. Katika kutekeleza masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi, Maafisa Masuuli wameendelea kutekeleza na kusimamia Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022- 2032) na Mwongozo wa Biashara ya Kaboni wa Mwaka 2022. Hata hivyo, imebainika kuwepo kwa uelewa mdogo kuhusu utekelezaji na usimamizi wa miongozo hiyo.

p) Uwekezaji wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi

71. Maafisa Masuuli wameendelea kutenga fedha kwa ajili ya maandalizi ya miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

q) Masuala ya Haki Jinai

72. Maafisa masuuli wanaohusika katika mnyororo wa haki jinai wameendelea kutekeleza mikakati ya kusimamia masuala ya Haki Jinai kwa kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wanaounda mnyororo wa haki jinai ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa weledi na ufanisi, kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo kwa watumishi na kuendelea kuelimisha jamii kuhusu masuala yanayohusu haki jinai ikiwemo ukatili wa kijinsia. Aidha, maandalizi ya usanifu na ujenzi wa Mfumo Jumuishi wa Kielektroniki wa Taasisi za Haki Jinai yamefanyika.

r) Uzingatiaji wa Maelekezo Mahsusi kwa Taasisi na Mashirika ya Umma

73. Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma yameendelea kutekeleza maelekezo mbalimbali ya Serikali kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayotolewa na Serikali. Taasisi na Mashirika hayo yameendelea kutenga na kuwasilisha mapato yasiyo ya kodi yakijumuisha gawio na michango ya asilimia 15 Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mujibu wa Sheria; Kufanya tathmini ya Utendaji wa Bodi za Wakurugenzi, na taarifa hizo kuwasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi na Mashirika yameendelea kuwasilisha Mipango ya Biashara na Sera za Gawio, na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea kuzipitia na kuziboresha kwa lengo la kuboresha viwango vya mgawanyo wa gawio vinavyowekwa kwenye Sera hizo.

74. Pamoja na hayo, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa Taasisi za Umma, ikiwa ni pamoja na kuboresha Muundo na Mgawanyo wa Majukumu wa Ofisi, sambamba na kuifanyia maboresha Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili iweze kusimamia ipasavyo Uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma; Kufanya tathmini ya kina kuhusu utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma 248. Tathmini hiyo ilipelekea Serikali kufikia maamuzi ya kuunganisha Mashirika na Taasisi 14 na kufuta na/au kurekebishwa kimuundo Mashirika na Taasisi za Umma tatu (3).

s) Uzingatiaji wa Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa

75. Ofisi za Wakuu wa Mikoa zimeendelea kutenga bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizopo. Vilevile, Ofisi hizo zimeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya kwa kutenga fedha za ununuzi wa magari pamoja na ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa. Zoezi la usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo pamoja na uibuaji wa vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa limeendelea kutekelezwa. Aidha, maandalizi na utekelezaji wa zoezi la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2024 yameendelea kufanyika.

t) Uzingatiaji wa Maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

i. **Mgawanyo wa Mapato ya Ndani:** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetenga jumla ya shilingi bilioni **541.25** kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia **39.91** ya bajeti ya mapato ya ndani kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Uchangiaji wa Miradi ya Maendeleo

S/N	Daraja la Halmashauri	Idadi ya Halmashauri	Asilimia ya Kuchangia	Kiasi kilichotengwa (shilingi bilioni)
1	Daraja la Kwanza	9	70	254.25
2	Daraja la Pili	17	60	94.66
3	Daraja la Tatu	102	40	163.55
4	Daraja la Nne	56	20	28.79
	Jumla	**184**	**-**	**541.25**

a) Shilingi bilioni 41.32 zimetengwa na Halmashauri 41 zikiwemo za daraja la kwanza (9), la pili (14) na la tatu (18) kwa ajili ya kuchangia ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara zinazosimamiwa na TARURA.

b) Jumla ya shilingi bilioni 100 sawa na asilimia 10 ya mapato yasiyolindwa ya shilingi bilioni 1,000 kwa halmashauri 184 zimetengwa kwa ajili ya utoaji wa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

c) Maelekezo yaliyotolewa kwa halmashauri kutenga asilimia 20 ya mapato yanayotokana na kilimo hayakuzingatiwa kikamilifu ambapo halmashauri zilitenga wastani wa asilimia 16.51. Kwa upande wa sekta ya mifugo maelekezo ilikuwa kutenga asilimia 15 ambapo halmashauri zilitenga wastani wa asilimia 11.12. Aidha, kwa upande wa sekta ya uvuvi, halmashauri zilivuka lengo kwa kutenga asilimia 12.56 ikilinganishwa na lengo la kutenga asilimia 5. Hali hii inaonesha kuwa halmashauri hazikutenga bajeti za kilimo na mifugo kama ilivyoelekezwa kwa kuzingatia mgawanyo wa asilimia.

ii. **Uzingatiaji wa Maelekezo kuhusu kutenga fedha kwa ajili ya Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Ardhi, Biashara, Viwanda, Uwekezaji, Maliasili na Mazingira:**

a) Shilingi bilioni 419.92 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya. Miradi iliyotengewa fedha ni ujenzi na ukamilishaji wa hospitali 118**,** vituo vya afya 146**,** ujenzi na ukamilishaji wa zahanati 290, ujenzi na ukamilishaji wa vichomea taka 26 na ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati.

b) Jumla ya shilingi bilioni 21.74 zimetengwa kwa watoto 9,484,171 katika halmashauri zote 184 ikiwa ni zaidi ya shilingi 1,000 kwa kila

mtoto chini ya miaka mitano zinazopaswa kutengwa kwa mujibu wa Mkataba wa Lishe wa Mwaka 2017.

c) Takwimu kwa ajili ya kuwezesha utengaji wa bajeti ya Elimumsingi na Sekondari (Kidato cha V na VI) ziliandaliwa na kuwezesha utengaji wa bajeti ya elimu bila ada na bajeti ya mishahara ambapo jumla ya shilingi bilioni 645.49 zilitengwa. Kati ya hizo, shilingi bilioni 243.85 ni za kugharamia mitihani na shilingi bilioni 401.64 za elimu bila ada;

d) Shilingi bilioni 521.19 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kukamilisha na kukarabati miundombinu ya shule, kuimarisha masuala ya malezi na makuzi, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni na nyumbani, kuwezesha michezo shuleni, kutoa nyenzo za kujifunzia na kufundishia hususan vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum, usalama wa mtoto na unasihi.

e) Shilingi bilioni 84.47 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa vitega uchumi 64; ujenzi wa vituo vya biashara; uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda 21; ujenzi na uboreshaji wa maeneo ya wafanyabiashara ndogo ndogo (Machinga), minada 55, masoko ya biashara 135, stendi 92 za mabasi na malori; ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa kumbi 15; kupima maeneo mawili ya uwekezaji; na ununuzi wa vitalu vya madini.

f) Shilingi bilioni 3.22 zimetengwa kwa ajili ya usimamizi na uendelezaji wa maliasili na mazingira ikiwemo: utunzaji misitu, hifadhi, vyanzo vya maji na maeneo oevu; uendelezaji na utangazaji wa vivutio vya utalii; upandaji miti; uzoaji na uondoshaji wa taka; na kuhakikisha teknolojia za uzalishaji zinazingatia uhifadhi wa mazingira.

g) Shilingi bilioni 25.79 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Sekta ya Ardhi na Mipango Miji. Miradi hiyo inajumisha miradi 67 ya utwaaji wa ardhi kwa kuwalipa fidia wananchi, miradi 43 ya mipango miji na miradi 24 ya kupima na kuuza viwanja kwa wananchi.

u) Ufuatiliaji na Tathmini

i. **Uimarishaji wa Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini**

Serikali imeendelea kuimarisha Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini kwa kuvitengea bajeti na kuvipatia watumishi na vitendea kazi ili viweze kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

ii. **Uzingatiwaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini**

Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu katika utekelezaji wa mipango na bajeti za mafungu yao kupitia Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini.

iii. **Uzingatiwaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo** (**NPMIS)**

Mafungu yameendelea kutumia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS) hususan katika uingizaji wa taarifa za miradi.

Kiambatisho Na. 1E

MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2025/26 - 2027/28

Maelezo ya Kisera kwa Ufupi

(i) Maelezo ya Waziri/Mkuu wa Mkoa/Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri/Mwenyekiti wa Bodi/Baraza

(ii) Maelezo ya Afisa Masuuli.

Sura ya 1: Uchambuzi wa Hali Iliyopo

1.1 Uchambuzi wa Wadau

1.2 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto

1.3 Masuala Muhimu ikijumuisha mawasilisho ya usimamizi wa vihatarishi

Sura ya 2: Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

2.1 Mapitio ya Utekelezaji - 2023/24

2.1.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2023/24

2.1.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi

2.1.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi

2.1.4 Muhtasari wa Malengo yaliyopangwa yakilinganishwa na Malengo yaliyofikiwa

2.2 Mapitio ya Utekelezaji kwa Nusu Mwaka - 2024/25

2.2.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2024/25

2.2.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi

2.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi

2.2.4 Muhtasari wa Malengo kwenye MTEF yakilinganishwa na Mafanikio yaliyopatikana

2.3 Changamoto zilizojitokeza 2023/24 na Mikakati ya kukabiliana na changamoto

Sura ya 3: Makadirio ya MTEF (2025/26 - 2027/28)

3.1 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.1)

3.2 Malengo Makuu, Shabaha na Shughuli zitakazofanyika (Fomu Na. 3A)

3.3 Makadirio ya Matumizi ya Mengineyo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na. 3B)

3.4 Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida (Fomu Na. 3C)

3.5 Makadirio na Maoteo ya Mapato (Fomu Na.4)

3.6 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.6)

3.7 Muhtasari wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (Fomu Na. 6.1)

3.8 Mfumo wa Matokeo wa Kitaasisi (Fomu Na.7)

3.9 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa kila Fungu (Fomu Na. 8A)

3.10 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa Kifungu (Fomu Na. 8B)

3.11 Kipengele Na.I – Muhtasari wa Wafanyakazi Walio kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Fomu Na. 8C)

3.12 Kipengele Na.II - Muhtasari wa Watumishi Wenye Kibali Wanaotarajiwa Kuajiriwa Katika Mwaka husika (Fomu Na. 8D)

3.13 Kipengele Na.III - Muhtasari wa Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kuajiriwa (Fomu Na. 8E)

3.14 Orodha ya Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kustaafu (Fomu Na. 8F)

3.15 Jedwali la Mishahara kulingana na Ikama (Fomu Na. 9)

3.16 Fomu ya Taarifa za Miradi (Fomu Na. 10A)

3.17 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Miradi kwa mwaka unaofuata kwa Fungu (Fomu Na. 10C)

Kiambatisho Na. 1F

RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

JINA LA FUNGU .....

FUNGU NA .....

RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

Imetayarishwa na;

Anuani ya Fungu

Machi, 2025

YALIYOMO

VIFUPISHO

SURA YA KWANZA

1. UTANGULIZI

1.1. Dira

1.2. Dhima

1.3. Majukumu ya Fungu

SURA YA PILI

2. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU YA MWAKA 2024/25

2.1. Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati…

2.2. Tathmini ya Utekelezaji Bajeti hadi Februari 2025

2.2.1. Taarifa ya Fedha Zilizovuka Mwaka 2023/24 (**Jedwali Na. 1**)

2.2.2. Mapato/Maduhuli (**Jedwali Na. 2**)

2.2.3. Matumizi ya Kawaida

2.2.4. Miradi ya Maendeleo

2.3. Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti

2.4. Changamoto (kama zipo) ambazo ni muhimu Kamati ya Bunge ikazifahamu na Mikakati ya Kuboresha Utekelezaji wa Bajeti

SURA YA TATU

3. MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2025/26

3.1. Vipaumbele vya Mpango na Bajeti

3.2. Makadirio ya Mapato

3.3. Makadirio ya Matumizi ya kawaida

3.3.1. Kazi zitakazotekelezwa (kifungu kwa kifungu) (**Jedwali Na. 3**)

3.4. Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

3.4.1. Miradi Itakayotekelezwa (**Jedwali Na. 4**)

3.5. Muhtasari wa Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2024/25 (**Jedwali Na.5**)
Muhtasari uoneshe maombi ya fedha kwa Fungu husika na mchanganuo wake

Jedwali Na. 1: Taarifa ya Fedha Zilizovuka Mwaka ….

Geresho la Mradi	Jina la Mradi	Shughuli zilizoombewa Kibali	Fedha zilizovuka Mwaka 2023/24		
			Fedha zilizobaki Kufikia Juni, 2023	Fedha zilizotumika hadi Feb 2024	Kazi zilizotekelezwa
5401	Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya		68,213,114	45,490,000	Fedha zimetumika kukamilisha shughuli za kuweka tiles, kupaka rangi, kuweka milango na madirisha,

Jedwali Na. 2: **Tathmini ya Ukusanyaji Mapato ya Ndani / Maduhuli**

Mapato Yaliyoidhinishwa	Makusanyo Halisi	Ufanisi (Asilimia)	Sababu za Ufanisi

Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida Mwaka …

Geresho la Kifungu: Mfano 1001

Jina la Kifungu: Mfano Utawala na Rasilimali Watu

NA.	KASMA	MAELEZO YA KASMA	KIASI KILICHOTENGWA		MAELEZO YA MATUMIZI
			2024/25	2025/26	
1.	21111	Mishahara ya watumishi	500,000,000	600,000,000	Kitengo kinaomba kuidhinishiwa **shilingi 600,000,000** kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi 30 walio katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni. Kasma hii imeongezeka kwa **shilingi 100,000,000** kutokana ongezeko la watumishi watatu (3) katika kitengo.

Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Maendeleo Mwaka …

Geresho la Kifungu: Mfano 1001

Jina la Kifungu: Mfano Utawala na Rasilimali Watu

Geresho la Mradi	**Jina la Mradi**	**Shughuli zilizopangwa kutekelezwa**	**Gharama za Mradi**	
			Fedha za ndani	**Fedha za nje**
4321:	Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (Primary Education Development Programme)	Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) Awamu ya Pili – GPE LANES II	-	2,000,000

Jedwali Na. 5: Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka….

Maelezo			**Bajeti 2025/26**
1	Matumizi ya Kawaida	Mishahara	
		Matumizi Mengineyo	
	Jumla Ndogo		
2	Matumizi ya Maendeleo	Ndani	
		Nje	
	Jumla Ndogo		
Jumla Kuu			

Kiambatisho Na. 1G

MUUNDO WA TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI

Ukurasa wa juu
Yaliyomo
Vifupisho vya maneno

Utangulizi
Sehemu hii itahusisha maelezo mafupi juu ya wajibu na majukumu ya Kamati katika usimamizi wa bajeti; orodha ya wajumbe na kumbukumbu za barua za uteuzi kwa mujibu wa sheria ya bajeti na orodha ya agenda zilizojadiliwa

1.0 Uendeshaji wa vikao
(Sehemu hii itahusisha ratiba na utaratibu wa uendeshaji wa vikao

2.0 Mapitio ya Muhtasari wa kikao cha kamati kilichopita
(Elezea kwa ufupi maazimio ya kikao kilichopita)

3.0 Ukusanyaji wa mapato na mgawanyo wa rasilimali:
- 3.1 Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato
- 3.2 Mgawanyo wa rasilimali kulingana na vipaumbele vya bajeti kama ilivyoainishwa kwenye mpango kazi (Bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo)
- 3.3 Utaratibu wa ugawaji wa rasilimali kila mwezi kulingana na vipaumbele vya bajeti
- 3.4 Mgawanyo wa rasilimali fedha katika Idara na Vitengo

4.0 Taarifa ya kazi zilizotekelezwa nje ya mpango na bajeti
5.0 Mafanikio, Changamoto na Mapendekezo
6.0 Hitimisho